# *MASWALI NA MAJIBU*

...maswali haya hapa kabla sijaenda mimbarani, lakini Ndugu Moore, yeye alinipigia simu ya ghafla, nami nilidhani mtu fulani alikuwa mgonjwa sana, naye alitaka tu mkutano. Kwa hivyo nilikuwa najaribu kummwondosha kwenye simu pale. Yeye alitaka nije katika wakati wa kutoa shukrani niwafanyie mkutano kule—kule Louisiana. Mwaka uliopita tulipokuwa kule, sisi—Bwana alianzisha mkutano wa ufufuo, na haujakwisha bado; ungali unaendelea. Ule mkutano wa ufufuo. Nasahau ni mia ngapi wameokolewa huu mwaka uliopita, wakati huo—baada ya mkutano huo wa ufufuo kule.

2 Sasa, nadhani inashangaza, labda, kuwa hapa asubuhi hii; na inashangaza kwangu. Nami sikujua, kwa hivyo hatukuutangaza miongoni mwa, mwajua, watu, nilikuja humu kujibu maswali kadha. Nilidhani hivyo...Kwa kawaida mchungaji aweza kuona kipi kilicho mioyoni mwa watu wake anapouliza maswali. Basi kwa njia hiyo tunaona yale watu wanayowazia.

3 Nami naamini kabla hatujaanza asubuhi ya leo, kulikuwa na mtu fulani aliyesema walikuwa na mtoto mchanga wa kuwekwa wakfu.—Billy alikuwa akiniambia kuwa kulikuwa na kuwekwa wakfu kwa mtoto mchanga. Ikiwa ndivyo, naam... Vema. Tutamleta mtoto huyo hapa na kumweka wakfu kwa Bwana; ndiposa tutajibu maswali hayo, kisha tutawaombea wagonjwa.

4 Nataka kutoa habari kwamba mama yangu ako tu karibu kama kawaida. Yeye...Sidhani yeye ni mahututi zaidi, ijapokuwa wanadhani hivyo. Lakini sidhani hivyo; naamini yeye yu karibu tu kama alivyokuwa. Na hadi Mungu atakaponiambia kuwa yeye yuafa; sitaamini hilo. Nitazidi kuamini kwa ajili ya Mama (ona?), hata Yeye atakaponiambia ya kwamba yuafa.

5 Naam, huenda anamchukua; sijui. Yeye...Huenda amenificha hayo nisije nikawa na wasiwasi na kadhalika; lakini nitaamini kuwa Mungu atamruhusu apone haijalishi yeye yukoje. Yeye hajakula kwa majuma matatu, ila tu maji ya sukari, lakini naamini yeye atapona haidhuru, Ona?

[Ndugu Branham amweka wakfu mtoto mchanga—Mh.]

6 Sasa, katika maswali tunayo machache yayo hapa, na sikupata hata nafasi ya kuyachunguza kwenye Maandiko ambayo—ya maswali yaliyoulizwa; kwa sababu nilipewa tu asubuhi hii. Nami niliyachukua tu muda mchache uliopita, nikayachukunguza-chunguza machache upesi upesi, na kuona maswali hayo, na kushangaa tu jinsi...Na baadhi yake... Hili ni kundi gumu zaidi nililowahi kulipata. Kwa hivyo

nilipo—nilipoyachunguza, niliona tungekuwa na wakati mgumu kwa haya.

7 Kwa hivyo nisipoyajibu kulingana na imani zenu katika maswali haya. . .Sasa, daima kumbukeni kuwa ni kadiri nijuavyo mimi. Ndiposa wakati mwingine labda mimi—kwa hivyo nitataja Andiko kuyajibu na huenda nisiwe na wakati wa kulisoma. Basi mwendapo nyumbani, yachunguzeni muone. Na kama nimemnukuu vibaya, vema basi, ni—nitakuwa nimekosea. Sikusudii kumnukuu ye yote vibaya, lakini—kunukuu vibaya Maandiko, lakini—kunukuu vibaya Maandiko, lakini wakati mwingine huenda tukafanya hivyo. Labda neno ambapo ingekuwa jambo fulani, ndipo huenda tukalisema kwa njia nyingine. Mwajua jinsi ilivyo rahisi kufanya hivyo.

8 Lakini tuna shabaha—shabaha yetu ni kuyanukuu moja kwa moja. Na kama ningeyachukua Jumapili hii na kuyajibu Jumapili ijayo; basi ningekuwa na nafasi ya kuyachunguza juma nzima.

9 Lakini kuna wagonjwa wengi wanaokuja, nami bila shaka nimekuwa na shughuli nyingi sana na sijapata nafasi ya ku—kuenda na kupiga baadhi ya simu zangu. Nami nilidhani leo ingekuwa wakati mzuri, kuwaacha wagonjwa waje humu maskanini tuwaombee. Nasi twajua kuwa maombi hugeuza mambo.

10 Maombi hutufanyia sisi jambo fulani. Nami leo naishi kwa maombi. Ninaishi kwa neema ya Mungu kwa maombi. Na asubuhi hii nikiwa nimechoka kidogo na ni mdhaifu, nataka sana maombi yenu, mnakaniombee.

11 Ndiposa nilikuwa nyumbani mwa rafiki yangu jana, nyumbani mwa Mkristo ambapo kulikuwa na Wakristo vijana waliokusanyika. Nami nilikuwa nikiongea nao, na lile—jambo fulani likanijia mimi, wazo kuhusu. . .Nilikuwa natazama mwituni na kwenye miti na nikaona ikifa, nami nikawazia, "Miti hii ni mizuri jinsi gani ijapokuwa inakufa; hata hivyo ni mizuri." Na wakati mwingine mti huonekana bora sana unapokauka kuliko wakati u wa kijani kabichi na bora sana. Nami nashangaa kama hilo halionyeshi hali yetu mbele za Baba yetu aliye mbinguni, maana Yeye alisema, "Machoni pa Bwana vifo vya watakatifu Wake ni vya dhamani."

12 Jinsi yapasa hilo liwe jambo zu—zu—zuri kwa Baba kumtazama mtoto Wake akija nyumbani Kwake huku anashikilia mahali pake katika Kristo, imani yake na maungamo yake (ona?), "Nimeokolewa kwa neema ya Mungu!" na kusimama pale (ona?) katika kufani, hali twaweza kushikilia maungamo yetu, tumeokolewa.

13 Nami naamini kuwa Baba yetu ni—hupenda ushujaa wetu na kuamini na kushikilia ushuhuda wetu. Na si—si kushuhudia tu unapojisikia mzuri, na mwenye afya, na mwenye nguvu;

ni wakati umelemewa, mdhaifu, na una shida. Hapo ndipo ushuhuda wako una maana.

14 Na tukiwazia juu ya hilo, nilikuwa nawaza hili, kuwa kifo hakishirikiani na uhai. Uhai na kifo haviwezi kudumu wakati mmoja. Nayo miti haina budi kutokwa na utomvu kabla majani hayajakauka mtini. Kwa hivyo basi, kifo kinashirikiaria—ningedhani katika mazingira ya wanadamu—kifo kinashirikiana na dhambi. Kwa sababu kabla hapajakuwepo dhambi yo yote, hatukuwa na kifo kamwe. Bali palipo mauti, pana dhambi; na palipo dhambi, pana mauti; kwa sababu mauti ni matokeo ya dhambi.

15 Ndiposa, yeye ambaye. . .Nafsi itendayo dhambi, itakufa. Lakini tunapozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, tuna Uzima wa Milele na hatuhusiani po pote na mauti. Ona? Mauti haiwezi kushirikiana na Uzima. Uzima hauwezi kushirikiana na mauti.

16 Basi nilipokuwa nikiwazungumzia wale—katika chumba kile jana ambapo Wakristo wadogo walikuwa, nilisema, "Kama mlikuwa mmesimama nje hapa barabarani na motokaa ilikuwa ikija barabarani kwa mwendo wa maili tisini kwa saa na haiendeki, ungeondoka barabarani upesi uwezavyo. Ungeruka, uikimbie, ufanye lo lote, kuondokea motokaa hiyo." Basi hivyo ndivyo dhambi yapasa iwe kwa Mkristo, kwa sababu dhambi inashirikiana na mauti. Na mara tu uonapo dhambi katika umbo lo lote, ruka ukimbie, iondokee. Sijali utakalofanya, kimbia ubaya wa kila namna. Kwa sababu kumbuka, kushiriki dhambi ni mauti. Ni kama tu kusimama pale na kuacha motokaa hiyo ikugonge.

17 Usingoje tu kuona yale itakayofanya; iondokee. Ubaya wa kila namna, jitenge nao upesi. Unapoona majaribu yakija, na dhambi. . .Unajua, kama ni jambo baya, hiyo mauti inakuwinda. Ona? Basi iondokee upesi, uwezavyo kuiondokea mo—motokaa inayokuja kwa maili tisini kwa saa. Ona? Unge—ungetaka kuiondokea upesi sana, kuondoka njiani. Ruka, ikimbie, kimbia upande wo wote, iondokee tu.

18 Na jinsi tujuavyo kuwa tuna Uzima, ni kwa sababu tunachukia dhambi. Nasi twachukia dhambi sana, hata twajua kuwa kuna mauti inayohusika pale, nasi tunajitenga na ubaya wa kila namna. Kwa njia yo yote tunayoweza kuiondokea, tunaruka, tunaikimbia, lo lote tuwezalo kufanya kuitoroka dhambi, kwa sababu dhambi ina mauti ndani yake. Nasi hakika hatutaki kuhusiana na cho chote katika mauti. Tunataka kuwa mbali nayo.

19 Kwa hivyo nilidhani hilo lingekuwa wazo ndogo nzuri. Lilinipata jana nikiongea na hawa Wakristo; nami niliwaza kuwa ingekuwa heri kueleza kanisa asubuhi hii, hasa wakati

vijana wameketi humu na kupitia—hupitia katika majaribu kama hayo.

20 Ndiposa, naamini swali, kama twaweza tu kulipata humu, jambo linalohusiana na hayo pia—Na kumbuka tu kuwa cho chote ambacho ni dhambi, mauti iko papo hapo. Na unaposhiriki dhambi hiyo, unashiriki mauti, kwa hivyo usiikaribie.

21 Na dhambi ni nini? Kutokuamini. Enhee! Usikaribie kutokuamini, cho chote kisichojali Biblia. Cho chote kisichojali Neno la Mungu, kiondokee! Na nikimaliza haya kabla sijawa na ibada yangu ya uponyaji, nataka kuongea kuhusu hilo, kutokuheshimu.

22 Sasa, kabla hatujajibu maswali au kujaribu hayo, hebu na tuombe. Baba yetu uliye mbinguni, tunaingia katika uwepo wako asubuhi hii katika Jina la Yesu, tukidai kuwa tumekataa kujitangamanisha wenyewe na vitu vya ulimwenguni, ambapo Yeye amesema, kuwa huwezi kumtumikia Mungu na mali, maana yake ulimwengu; au tutamchukia mmoja na kumpenda mwingine au kumpenda mmoja na kumchukia mwingine.

23 Nasi twaamini asubuhi hii kuwa sisi tu wanaoshirikiana na Uzima wa Milele tunapomkubali Yesu Kristo kwa imani na tuna ushuhuda wa Roho Mtakatifu akiishi maishani mwetu akituongoza. Tuna shukrani nyingi sana kwa ajili ya hili, kuwa tuonapo dhambi haijalishi ni ya uvuguvugu vipi, inaonekana nzuri vipi, kuna kitu fulani ndani yetu kitufanyacho turuke, kuiondokea, kama tu mfano niliotoa kuhusu motokaa ijayo kwa mwendo wa kasi sana. Hatutaki kupatwa po pote katika—dhambi. Iondokee.

24 Na sasa, Bwana, najisikia asubuhi hii kuwa kunao wengi wagonjwa na wenye mahitaji, ningewaombea, Bwana, kuwa utawapa imani hasa hawa katika maskani haya asubuhi hii watakaoingia kwa mstari wa maombi, wapate kuweka kando kila mzigo mzito, kila—kutokuamini kwote, wayaache upesi, na wamkimbilie Bwana Yesu katika imani wakaamini.

25 Nawaombea wale walioko mahospitalini na katika vituo vya matibabu. Pia, Bwana, naomba kwa ajili ya mama yangu. Mpaka sasa, Bwana, Wewe umemdumisha pamoja nasi, na tunakushukuru kwake. Na kwa imani tunainyosha mikono inayohitaji, kwanza kujua mapenzi ya Mungu, kuona kama ni mapenzi Yake kwake Kwenda. Kama ni mapenzi Yako, basi sisi tu—hayo ni mapenzi yetu, lakini kwanza tunataka kujua kama Shetani amefanya uovu huu na linatendeka kwa manufaa ya wale watupendao katika kutujaribu. Basi, Bwana, tunataka kusimama kishujaa mahali pa wajibu wetu.

26 Twaomba asubuhi hii, baba, kukumbuka huo wito wote wa simu na maombi maalum yaliyoko pale afisini yakingoja. Wabariki marafiki wetu kila mahali.

27 Na leo kura imeangukia wakati wa kujibu maswali, Bwana, twatambua kuwa haya ni ya kilindi, mambo manyofu yaliyo kwenye mioyo ya watu. Hawakuyauliza kipuzi; waliyauliza kwa sababu wana hamu katika kujua Kweli. Neno Lako ni Kweli.

28 Kwa hivyo, Baba, twaomba kuwa Wewe utahusisha nia zetu asubuhi hii katika Kweli hii, lile Neno, na utusaidie, Bwana, tuweze kufahamu vema leo tunapoondoka katika nyumba hii ya kufunzia, ili iwe nzuri kwa nafsi zetu. Twaomba haya kwa utukufu wa Mungu katika Jina la Yesu Kristo Mwanawe. Amina!

29 Sasa, kuna leso zilizowekwa hapa, nadhani, ziombewe, nasi tutafanya hayo mara moja upesi tu tuwezavyo. Sasa, wakati tulio nao ni karibu saa moja na nusu. Sijui hasa, kama nilivyosema hapo mbeleni, nitaweza kuyajibu maswali haya yote au la. Lakini yale tumepanga leo ni kuyajibu maswali, kisha tupate mahubiri madogo hapa kwa—kwa kusaidia imani ya watu, halafu tuwaombee wagonjwa. Basi kumbukeni ibada ya usiku huu, na mkutano wa maombi wa katikati ya juma, mkutano wa wanaume, na kadhalika.

30 Nami sijui Jumapili inayokuja kama . . . Nina somo moyoni mwangu ambalo ningetaka kuleta kanisani ikiwezekana, Bwana akiruhusu, Jumapili ijayo, jambo mu—muhimu mno lililonijia juma hili kuhubiri, ujumbe tu wa kuhubiri, ujumbe wa uinjilisti . . . Tutaona hayo baadaye kidogo Bwana wetu atakavyotuongoza.

31 Basi mniombee sana, kwa sababu yapasa uamuzi fulani utolewe. Ndugu Roy Borders (nadhani yeye anaketi mahali fulani ndani humu asubuhi hii), yeye hushughulikia mikutano, naye ana kitabu kimejaa mialiko iliyoletwa katika miezi michache iliyopita—ya kwenda mahali mbalimbali, pia watu watamwalika mikutanoni. Na kwa hivyo ombeni kwamba Mungu ataniruhusu mimi kutoa uamuzi sahihi. Kusudi cho chote nifanyacho, kiwe sahihi, ki—kifaacho.

32 Sasa, kujibu maswali ambayo twajua ni makali . . . Na hiyo ndiyo sababu mimi hujibu maswali. Hatukutangaza ibada ya uponyaji au cho chote kile, kwa hivyo itakuwa tu watu wa nyumbani hapa; tupate kuona yaliyokuwa mioyoni mwao.

33 Na Ndugu Neville anayeketi pale nyuma, ndugu yetu mpendwa na mchungaji, yeye—nina shukrani kumwona yeye akiendelea katika Ufalme wa Mungu; naamini yeye ameendelea mbele sana katika miaka miwili iliyopita kuliko alivyowahi kufanya katika mingine yote . . . ? . . . ikiwekwa pamoja. Jinsi Bwana amembariki. Nina furahia hayo sana.

34 Na nitasema si mbele zake tu . . . nafanya hivyo asipokuwepo, nanyi mwajua hayo. Nilimjua Ndugu Neville tangu nilipokuwa mvulana. Ona? Nami najua kuwa kama Ndugu Neville . . . naamini hili; yeye hukosea kama sisi wote tufanyavyo; sisi—sisi

sote hufanya hayo, sisi tungali wanadamu. Lakini halingetoka moyoni mwake; siamini hivyo. Yeye angekuwa mnyofu, naye kila mara amekuwa mwenye moyo mweupe sana.

35 Naye aliposhika huu Ujumbe, nimekuwa naye—aliletwa hapa kwa kura za kanisa awe mchungaji hapa wakati hata hakufahamu mambo haya kama anavyofahamu sasa. Lakini unyofu wake wa moyo kupenda kuketi na kuyachunguza na kuyaendea kwa unyenyekevu, hata nadhani yeye ana msimamo mzuri na thabiti, hata yeye asimamapo sasa, yeye ajua anaposimama sasa.

36 Kwa hivyo nina—nina furaha tele kwa maskani haya. Nao walisema usiku uliopita katika ule—wao walikuwa na mkutano hapa kama watajenga maskani mapya au wayaongeze haya na kuyapanua na kutengeneza vyumba vya shule ya Jumapili ndani yake; na kanisa kwa wingi lilipiga kura yapanuliwe, kuongeza sehemu mpya kwake hapa nje, kulifanya kubwa, zaidi, na kuweka vyumba vya shule ya Jumapili ili kuwe na madarasa kwa watu wote, na kutandika zulia sakafuni, na kuweka fito, kuijenga vilivyo, na matofali nje. Na kwa hivyo kanisa lilipigia hilo kura. Nami nafikiri waandishi wa ramani na wengineo wanafanya kazi sasa. Kuna mkutano wao kesho kulifanya kanisa ku—kubwa kidogo, kuliongeza upande wa nyuma na kulitengeneza vinginevyo kote. Kwa hivyo tutamshukuru Bwana kwa hayo.

37 Sasa, katika maswali haya mimi. . .Baadhi yake hata sijaangalia. Huenda ikanibidi kuchukua muda kuyaendeleza maneno haya kusudi nipate kuyajua. Si mwandiko wako, lakini ni uhaba wa elimu yangu.

**151. Twaamini katika kubatizwa. . .Matendo 2:38; lakini twawezaje kujibu watu kuhusu ule ubatizo mwingine? Je, wao wameokoka au la? Pia wale walioendelea na hawakupokea nuru hii?**

38 Sasa, hilo ni swali nzu—nzuri. Sasa, hebu niseme tena (ona?) kuhusu maswali haya, kama una—kama nisipoyajibu kulingana na mawazo yako. . .nitayajibu karibu sana na Maandiko kadiri nijuavyo, kuyafanya ya Kimaandiko.

39 Sasa, njia ya Kimaandiko ya ubatizo wa maji ni kwa Jina la Bwana Yesu Kristo, ambayo inapatikana katika Matendo 2:38 na penginepo, Biblia nzima. Na watu wengi siku hizi na karibu makanisa yote tangu mwanzo, lile lililouanzisha, walibatiza watu katika jina la Baba, jina la Mwana, na katika jina la Roho Mtakatifu. Sasa, wanafanya hivyo kwa kukosea. Hakuna agizo kama hilo katika Biblia, halipo po pote pale. Hata halipatikani katika Maandiko.

40 Petro alipo. . .Mathayo alipokuwa akiandika yale aliyosema Yesu. . .Ambapo wangechukua Mathayo 28:19, “Basi, enendeni,

mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi Wangu, mkiwabatiza kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu” . . .

41 Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, hivyo ni vyeo, si jina. Jina la baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni Bwana Yesu Kristo. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu . . . Na kama Yeye . . . Ndiposa wakabatiza kote Bibliani, kila mtu kwa Jina la—la Bwana Yesu Kristo. Kote katika historia waliendelea hadi kuanzishwa kwa Laodikia (samahani)—lile baraza la Nikea la kanisa Katoliki kule Nikea, Rumi.

42 Wakati kanisa la Pentekoste . . . makundi mawili, waligawanyika, moja lilitaka kukaa na Neno, Neno lililoandikwa, lingine lilitaka kanisa maarufu kabisa. Ilikuwa katika utawala wa Konstantini. Naam, Konstantini hakuna mtu wa kidini; yeye alikuwa kafiri tangu mwanzo. Lakini yeye—yeye alikuwa mwanasiasa aliyetaka kuunganisha . . . Nusu ya Rumi ilikuwa Ukristo; na nusu ilikuwa ukafiri, kwa hivyo yeye akaingiza baadhi ya ukafiri na baadhi ya Ukristo kwenye lile kundi maarufu; nao wakatengeneza dini yao wenyewe.

43 Kwa hivyo, kutokujali Biblia, kanisa Katoliki huamini ya kwamba Mungu alilikabidhi kanisa mamlaka ya kubadili au kufanya cho chote lilichotaka kufanya. Ona? Kwa hivyo, kama kanisa Katoliki ni sahihi, kama hayo aliyotenda Mungu ni kweli, basi sisi sote tumekosea isipokuwa Wakatoliki (ona?), kanisa Katoliki ni kweli. Ndipo kanisa Methodisti ndiyo kweli. Ndipo kanisa Baptisti ni kweli au madhehebu yote ni ya kweli. Ona? Wana haki. Na nani ana haki basi? Kama Wakatoliki wana mamlaka ya kubadili cho chote Biblia inachotaka kusema na kufanya mafundisho mengine kwa “Maria, mtakatifu” na kadhalika, Methodisti ina haki ya kusema, “Ubatizo kwa maji mengi si sahihi; sisi tutanyunyuzia,” na kila moja walo ni la kweli, kwa sababu kila mmoja aweza kufanya cho chote ambacho kanisa lishikiliacho, sasa, kanisa ni nani basi? Je, ni Methodisti, Bapsti, Presbiteria, Katoliki, au ni lipi? Ona?

44 Kwa hivyo huwezi—wajua kuwa Mungu, ambaye—ambaye ndiye asili ya hekima yote hangefanya kitu kama hicho. Hakuna . . . Hakuna hata busara kwake, sembuse busara ya viumbe vya kimbinguni. Kuna kitu kimoja ambacho ni sahihi; hicho ni Neno. Neno ni kweli!

45 Kwa hivyo basi, kama kanisa Katoliki lilitaka kusema asubuhi ya leo, “Tutafutilia mbali ubatizo kabisa na tuchukue kula kibonge cha sukari kila asubuhi. Tutakula hicho kwa ondoleo la dhambi!” ndipo hilo lapasa kuwa sahihi kwa sababu ni—Mungu alitoa mamlaka hayo kwa kanisa.

46 Lakini mwaona, kwangu Neno ndilo sahihi, kwa sababu mwishoni mwa Biblia, Mungu alisema haya katika Neno Lake, “Ye yote atakayeodoa neno moja toka kwa hiki au atakayeongeza

neno moja Kwake, yeye ataondolewa, sehemu yake, toka kwenye Kitabu cha Uzima." Kwa hivyo kwangu ni Neno!

47 Na hakuna kitu katika Biblia kama ye yote kubatizwa katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; kwa sababu hakuna kitu kama hicho. *Baba* si jina; na *Bwana* si jina; na *Roho Mtakatifu* si jina, lakini Jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu ni Bwana Yesu Kristo. Hayo ndiyo yale hasa mitume na kotekote katika zamani zile wametambua.

48 Sasa, swali linalofuata ni...Hakika hilo ni sahihi Kimaandiko. Hilo ni Kweli.

49 Na katika Biblia walipopata watu ambao walikuwa wamebatizwa kwa maji mengi kwa njia nyingine isipokuwa kwa Jina la Yesu Kristo, waliagizwa wabatizwe tena kwa Jina la Yesu Kristo kabla wao hawajampokea Roho Mtakatifu—Matendo 19:5. Sawa! Kwa hivyo hilo ni Kweli Kimaandiko.

50 Sasa, hakuna askofu; hakuna askofu mkuu; hakuna mhudumu; hakuna mwingine ye yote awezaye kusema neno moja dhidi ya hayo, kwa sababu hayo ni Kweli. Ona?

51 Nami niliuliza hivi majuzi kule Chicago mbele ya wahudumu mia tatu waliosimama juu pale kubishana na kuuliza kuwa... mimi...Na Bwana aliniambia, Yeye alinipa ono, kuniambia ambapo tungekuwa na yale ningefanya. Nilisimama mbele ya wahudumu mia tatu wa utatu, nami nikasema, "Sasa, kama nimekosea sana katika fundisho hili, baadhi yenu watu simameni hapa na nionyesheni ambapo nimekosea kwa Maandiko bila kitabu kingine. Kama hakuna kitu kama uzao wa nyoka au kitu kama hicho ambacho nimekuwa nikifundisha, njooni hapa tu mkanionyeshe kwa Maandiko." Hamna ye yote aliyejimundu (ona?), kwa sababu haiwezi kufanywa. Naam. Si kutofautiana, bali ni Kweli tu; ni Neno. Na hapo ndipo... Hamna ye yote awezaye kubishana na hilo; hilo ni Neno la Mungu; hakuna ye yote awezaye kufanya hivyo. Ona?

52 Lakini sasa, "Hawa ambao..." Hebu nisome hili ili niwe na hakika ni sahihi. Ona? "Kuhusu mabatizo mengine, wameokolewa au la? Pia wale walioendelea na hawakupokea kamwe nuru hii?"

53 Vema, naamini—naamini kabisa kuwa Mungu aliwaita watu Wake na kuchagua Kanisa Lake, na wale wote ambao wangekuwa humo, kabla kuwekwa misingi ya ulimwengu. Naamini Biblia hufundisha hayo. Nami naamini kuwa kila mtu anayempenda Mungu kwa moyo wake wote atatafuta Ukweli. Ni—ni—ninaamini hayo, kuwa wao watafanya hilo. Kila mtu anayempenda Mungu atafanya hayo.

54 Naamini kama mtu alibatizwa vibaya bila kujua, bila kujua yeye alibatizwa vibaya...Sasa, siwezi kusema hili Kimaandiko. Lakini naamini kwa moyo wangu kuwa kama mtu hakujua kutenda yaliyo kweli, naye alifanya kitu fulani

kadiri alivyofahamu, naamini kuwa Mungu hangemhesabia hayo na angemwokoa haidhuru, kwa sababu yeye hakuwa. . . Kumbuka, kule nyuma katika siku za Wesley, nyuma katika siku za Luther katika matengenezo yale, hao watu wakuu wa Mungu ambao Mungu aliwaheshimu na kuthibitisha kuwa Yeye aliwaheshimu, walikufa katika imani (ona?), wakiwa na Nuru yote waliyokuwa nayo.

55 Na naamini huenda kukawa bado kuna vitu kama. . .Kuna ye yote aliyemsikia Charles Fuller asubuhi hii kwenye "Saa ya Ufufuo wa Mtindo wa Kale?" Yeye ni mmoja wa walimu wangu wa Biblia niwapendao sana, bali yeye ni, ni mzee sana, na. . .Lakini nafikiri yeye ni mwalimu mashuhuri wa Biblia. Naye alisema asubuhi hii (yeye alikuwa akifundisha juu ya unabii, naamini); yeye alisema kuwa—kuwa kulikuwa na mambo makuu mbele, mambo ambayo kanisa halijui lo lote kuyahusu yangefunguliwa kwa watu. Nilisema, "Amina!" kwa hayo. Naamini kuwa bado tungali tuna Nuru kuu inayokuja sasa itakayojaza tu dunia hivi karibuni kwa muda mfupi, labda kwa miezi tu. Lakini naamini kuwa kuna Nuru kuu inayokuja.

56 Naamini kuwa mtu ye yote kwa imani yake na unyofu, na anayetembea katika Nuru yote aliyo nayo ataokolewa.

57 Kumbuka, katika kule kuja kwa Bwana Yesu, mwakumbuka jinsi Yeye alivyowapata wale waliotembea katika Nuru yote iliyowapasa watembee ndani yake? Mnakumbuka yale yaliyotendeka? "Si yeye ni mtu mzuri, hata Akida wa Kirumi, yeye amejengea mji wetu—au watu wetu sinagogi, naye (vitu hivi vyote ambavyo yeye alivyofanya)—yeye anastahili baraka hii anayoombewa." Ona, Mungu ni Baba anayefahamu; Yeye ajua moyo wako, kama unaona Nuru hakika au kama huoni Nuru; Yeye ajua.

58 Sasa, naamini hakika kwa moyo wangu wote kuwa jibu sahihi kwa swali hili ni kuwa ubatizo sahihi ni katika Jina Lake Yesu Kristo, na kwamba wale wote waliobatizwa kinyume na mioyoni mwao, si kwa uchoyo, wanasema tu, "Vema, sitaki kupumbazika nao!". . .Sasa mtu huyo, hilo litakuwa juu yao na Mungu. Lakini kama hawakujua vinginevyo, naamini kuwa wameokoka. Ni—ninaamini kwa moyo wangu wote, kwa sababu hawakujua vinginevyo.

Tungekaa kwa muda, muda mrefu kwa hilo, lakini tunajaribu kuyapata haya yote tukiweza.

**152. Tafadhali fafanua Waebrania 6:4 na 6, na pia fafanua Waebrania 10:26-39? Tafadhali eleza kama hili lahusu watu walio na Roho Mtakatifu au watu waliotakaswa; tafadhali eleza tofauti yake.**

59 Vema, hebu tuone ambapo mtu huyu anarejea, Waebrania 6 na 4. Napenda maswali ya Biblia ambayo—yanavuta kitu fulani ndani yako hata unapata—unapata kitu ambacho hungepata

vinginevyo. Kwa sababu una—unaona yale watu wengine wanayowaza, yale yaliyo mioyoni mwao (ona?), na unajua yale wanayotenda.

Sasa, kuna Waebrania 10, na hapa Waebrania 6 na 4. Vema.

> *Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washiriki wa Roho Mtakatifu.*
>
> *Na kulionja. . .neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo,*
>
> *Wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu, kwa kuwa wanamsulubisha Mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na kumfedhehi kwa dhahiri.*

Sasa hapo ni pamoja. Sasa, Waebrania 10:26. Vema, Waebrania 10 na 26.

> *Maana kama tukifanya dhambi kusudi baada. . .*
>
> *baada. . .ya kupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi;*
>
> *Bali kuna kuitazamia hukumu. . .kwenye kutisha, na ukali wa moto ulio tayari kuwala wapingao.*
>
> *Mtu aliyeidharau sheria ya Musa hufa pasipo huruma, kwa neno la mashahidi wawili au watatu:*
>
> *. . .haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu—imempasa,* mtu *aliyemkanyaga Mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo, na. . .kumfanyia jeuri Roho wa neema?*

60 Yote mawili yanahusu jambo lile lile. Sasa, ningetaka kumfafanulia haya m—mtu yule. Sasa, ukichunguza hapa katika Waebrania 6 na 4, ilisema, "Haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru". . .Hayo—hayo yanahusiana na Andiko hili lingine ambalo limekwisha somwa. Kama umekwisha kupewa nuru halafu uachane na nuru hiyo, haiwezekani kwa mtu huyo kupata mahali pake tena. Ona?

61 Sasa, Waebrania yaeleza tu adhabu iliyofuata kukataa huku. Jambo moja lililo baya mno ulimwenguni ni kumkataa Kristo, ni kukataa Nuru ya Maandiko.

62 Sasa, mnatambua, "Maana haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, wakianguka kuwafanya upya tena hata wakatub. . ." Ona? Basi. "Maana haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru, na kukionja (tazama), *kukionja* kipawa cha mbinguni. . ." Wamekuwa tu ukingoni wake: "kukionja kipawa cha mbinguni. . ."

63 Sasa, unaona hawakuwa wameshawahi kufikia ubatizo wa Roho Mtakatifu. Ona? Walipewa nuru kwake: "Na kukionja

kipawa cha mbinguni (ona?) lakini walifanywa washirika wa Roho Mtakatifu (kwa kukionja), na wamekwisha kuonja Neno zuri la Mungu, (sehemu yake, ona?) na nguvu za ulimwengu ujao, wakaanguka, haiwezekani kuwafanya upya tena . . . ”

64 Sasa, Waebrania 10 hapa yatupea tu hukumu ya hayo. “Yeye aliyedharau sheria za Musa hufa pasipo huruma kwa neno la mashahidi wawili au watatu. Mwaonaje, haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu aliyeikanyaga ile Damu ya Yesu Kristo na kuihesabu kuwa kitu ovyo waliyotakasiwa kwayo?”

65 Sasa, kuweka haya pamoja kufanya swali lile kwako, hebu tuchukue Andiko moja na mtu mmoja katika Biblia aliyefanya hili, ndipo tutaona.

66 Sasa, kanisa lote siku hizi ni mfano halisi wa mfano ule. Twajua hilo. Kuna mfano wa mfano halisi. Sasa, Israeli walipokuwa safarini toka kwenye nchi ya Palestina—toka Misri kuingia Palestina, ilikuwa mfano wa kanisa katika roho siku hizi safarini mwake kuelekea ile nchi ya ahadi . . . Ninyi nyote mwakubaliana na hilo, sivyo? Wanatheologia wote hukubaliana na hilo, huo ulikuwa mfano.

67 Wao waliondoka Misri. Misri ilikuwa ulimwengu. Waliondoka, wakapitia katika maji ya utengano kwenye ile Bahari ya Shamu kupitia kwa ubatizo, wakatokea upande wa pili wakifurahi na kumsifu Mungu, wakaenda kwenye—wakapata sheria, na toka pale wakashika njia kwenda katika nchi ya ahadi.

68 Vema, mlitambua kabla tu wao kuingia kwenye ile nchi ya ahadi (ona?) kabla wao kuingia katika ile nchi ya ahadi, ambayo ingechukua siku chache tu, siku kumi au kumi na moja, huenda si nyingi, kwa sababu ilikuwa tu maili arobaini na kitu. Wangelienda moja kwa moja hadi katika ile nchi ya ahadi, wangerudi moja kwa moja kupitia katika ile—miaka ile—kila—kila hatua ya safari ambayo tumepitia. Nao wakafika kule, wakavuka ile Bahari ya Shamu. Jeshi la Farao lilizamishwa nyuma yao. Wao walikuwa huru toka kwa adui zao, wakaanza kupitia jangwani, kufikia mpakani mwa nchi ya ahadi kule Kadeshi Barnea, kisha wao wakashindiwa hapo. Mbona? Mbona wao walishindwa?

Sasa, Musa aliwaambia wale makabila kumi, akasema, “Atatuma mtu mmoja toka kwa kila kabila kuwakilisha kila kabila, aende kupeleleza nchi ile kuona ilikuwa nchi ya namna gani.”

69 Sasa, kama hiyo si kamili hata—hata mahali pako asubuhi hii, ambapo umefikia. Leo wewe—kanisa limepitia katika kuhesabiwa haki kumpitia kwa Luther, likapitia kwa utakaso katika Methodisti, na sasa limefikia wakati wa ahadi. Ile ahadi ni ubatizo wa Roho ambao umeahidiwa kote katika Agano la Kale na Jipya pia (ona?), ile ahadi. “Tazama, nawaletea juu yenu

ahadi ya Baba yangu. . .” Petro alisema hayo kwenye siku ya Pentekoste.

70 Hiyo ndiyo ahadi. Nchi ya ahadi ni kuishi katika hii nchi ya Roho Mtakatifu. Hiyo ndiyo ahadi ya Mungu kwa kanisa, ni kuishi katika uwezo wa Roho. Ni ulimwengu mwingine; ni nchi nyingine. Yakupasa uondoke katika hali ambayo umekuwemo, kupokea ile ahadi. Kumbuka ile ahadi, “Mtapokea nguvu kutoka juu, akisha kuwajilia juu yenu, Roho Mtakatifu . . . ”

71 Na Petro alisema kuwa ahadi ile iliyofanywa kote katika Agano lile, la Kale na Jipya . . . Mna—mnaona ikiahidiwa hadi, iliahidiwa hadi siku hiyo ya Pentekoste, ndiposa wao wakaingia katika ahadi ile.

72 Naam, watu hao walikuwa wametoka na kuona ishara kuu na maajabu katika Israeli. Kisha yeye akatuma watu kadha nje kuipeleleza, mmoja toka kwa kila kabila. Na wengine wao walirudi kwa . . . Vema, wengine wao hawangevuka. Wawili walivuka. Waliporudi, walikuwa na kichala cha zabibu kilichohitaji watu wawili kukibeba. Sasa, hawakuwa wameshaonja kamwe. Walikuwa katika—wao walikuwa jangwani; na kwa hivyo, huko hakukuwa na mahali pa matunda na vyakula. Walilishwa kwa mana, chakula toka Mbinguni, na tomboo, na wanyama wa porini na vile walivyolishwa.

73 Lakini sasa wao walikuwa wanavuka kuingia ile nchi, nao walikuwa na kichala cha zabibu kilichokuwa kikubwa sana hata kilihitaji watu wawili kubeba zabibu hizi. Na hawa wawili walivuka wakaingia katika ile nchi ya ahadi na wakarudi na kumpa kila mmoja wa hao wengine ukingoni mwonjo wa zabibu hizi. Walifanyaje?

Waliporudi, badala ya kufurahi kwa sababu wao walikuwa wameonja zabibu zile, badala ya hayo, walirudi nyuma kwa makabila yao na kusema, “Ee, lakini tumeona ile miji mikubwa ya Wafilisti yenye kuta, au Wahiti, na Waperezi na wale—wale—na yale *makabila* mengine mbalimbali kule.” “Naam,” kasema, “wao ni Wanefili. Isitoshe, tunaonekama kama panzi wadogo kando yao. Hatuwezi kuitwaa nchi hiyo. Mbona ukatuleta nje huku haidhuru?” Ona? Na Biblia ilisema kuwa wao wote waliangamia jangwani, kila mmoja wao; walikufa. Walifanyaje? Wao walikuwa waamini wakwamia-mpakani. Walifikia kitu chenyewe na kuona ile ahadi, wakajisikia kuwa hawangeweza kuvuka na kuitwaa ile ahadi.

74 Sasa, hivyo ndivyo hasa imekuwa siku hizi kupitia kwa kuhesabiwa haki na kutakaswa. Ona? “Wameikanyaga ile Damu ya Yesu Kristo waliyotakaswa Kwayo,” ni wale watu waliotakaswa wanaokuja hata mahali ambapo wao huona ule ubatizo wa Roho Mtakatifu, nao wanageuka upande na kusema, “Ni uzushi; hatutaukubali. Tutafukuzwa nje ya makundi yetu; tutafukuzwa makwetu. Tutafukuzwa makanisani mwetu.

Hatuwezi kufanya hayo (ona?), kwa sababu ni kinyume cha mafundisho ya kanisa letu." Amehesabu ile Damu ya Yesu Kristo iliyomleta umbali huu wote, moja kwa moja hata kwa kutiwa muhuri kwa ile ahadi, kisha akaiondokea. Yeye alisema hawawezi kuokolewa kamwe. Ona, Ona? Si wale waliovuka na kuingia katika ile nchi ya ahadi . . .

75 Kumbuka, Yoshua na Kalebu waliokuwa ndio watu wawili pekee toka kwa kundi hilo lote la watu milioni mbili na nusu walioingia katika ile nchi ya ahadi, kwa sababu wao walivuka wakaingia katika ile nchi ya ahadi, na kupata baraka, na kurudi. Nao wakasema, "Tunaweza kuitwaa, kwa sababu Mungu alisema hivyo."

76 Nao wakakomea hapo. Mbona? Sasa, watu hao wote walikuwa wakitazama mambo yalivyo, lakini Yoshua na Kalebu walitazamia yale Mungu aliyosema: "Nimewapa ninyi nchi hiyo; enendeni mkaitwae."

77 Na ndivyo leo, watu husema, "Ee, nikibatizwa katika Jina la Yesu Kristo, nikimpokea Roho Mtakatifu, kama ninge— ningenena kwa lugha au unabii, au ningetoa ushuhuda au kupiga shangwe kanisani, wangenifukuza." Endelea mbele!

78 Unasema, "Vema, nitakwambia hivi sasa, naishi maisha ya Kikristo; naishi maisha mazuri, masafi, yaliyotakasika . . ." Naam, lakini umefikia shindano la kuamua, umefika mahali pale, pale mpakani. Na ukiyapa hayo kisogo, basi haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru . . . Ona?"

79 Kwa maneno mengine, mtu apitie kwenye kuhesabiwa haki, aenda, aseme, "Naamini nataka kuhubiri Neno." Yeye aokoke; akasema, "Nimechoshwa na dhambi." Vema. Ndipo yeye atoke nje, na kwanza yeye bado huvuta sigara, na labda yeye hutamani ama cho chote kile. Baada ya muda mchache yeye aseme, "Mungu, hili halimpasi Mkristo, hasa mhudumu, kuwatazama wanawake kwa njia mbaya, kuvuta sigara!" au; "Mimi hunywa pombe na wenzangu, lakini—na hata kusanyiko langu, bali halionekani sahihi. Nitakase, Bwana." Ndiposa Bwana anamtakasa, anaondoa hizo tamaa mbovu zote toka kwake, kila kitu. Ndipo yeye ni chombo kilichotakaswa. Ndipo kile Mungu ampacho yeye ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kufanya hivyo, yeye apaswa kuondoka katika kundi lile yeye alilo nalo. Hapo ndipo yeye aonyesha alivyo hasa; ndipo yeye aghairi. Yeye afanyaje anapoghairi? Akanyaga ile Damu ya Yesu Kristo iliyomtakasa, kama kwamba ilikuwa kitu ovyo kisichoweza kumvusha kule. Basi hawezi kuokolewa. Halafu inakuwaje? Kuuelekea ukali wa moto pamoja na ile hukumu.

Natumai hilo ni dhahiri. Kama sivyo, haya basi mnijulishe wakati mwingine. Nina mengine mengi hapa, mimi . . .

**153. Ndugu Branham, Yesu alikusudiaje katika Injili ya Yohana 21:15 hata 17 yeye alipouliza Petro kama yeye alimpenda**

**na kumwambia alishe wana kondoo Wake, kisha akasema, "Chunga kondoo Zangu!" na katika kifungu cha 17 yeye alisema tena, "Lisha kondoo Zangu?!"**

80 Vema, hiyo ni kusema hivi. Ona, Kristo ni Mchungaji. Yeye alikuwa akienda Zake, na Yeye alikuwa anaacha agizo kwa Kondoo Zake, ambalo mchungaji ye yote hulisha, ambao ni Kundi Lake, Kanisa Lake. . . Ona? Yeye alikuwa akiongoza—au akiacha agizo kwa hawa wanafunzi kuendelea kulisha kundi lile, ku—kuwa mchungaji, lisha kondoo.

81 Kwa maneno mengine hivi, uki—ukitazama nje hapa. . . Hapa asubuhi hii, hilo ndilo ninalofanya. Sasa, kondoo watakua tu jinsi unavyowalisha chakula cha kondoo sasa, ukipika sambusa kubwa ukampe kondoo, hawezi kukulia hicho, kwa sababu, ona, yeye si—hicho si chakula cha kondoo. Ona? Na—na kama ungekaangaa au ku kuwa na minofu mizuri ambayo imetayarishwa, na kuwapa kondoo, si—si chakula cha kondoo. Yeye hangekila, hivyo tu, kwa sababu yeye ni kondoo. Lakini kondoo hupenda chakula cha kondoo. Vema basi, unapohitajika kulisha kundi la Mungu, usililishe kwa theologia iliyotengenezwa na wanadamu; lilishe Neno; hapo ndipo kondoo watakulia. Walishe Neno!

82 Kuwa mchungaji, mchungaji halisi. "Lisha Kondoo Zangu." Wana-kondoo ni wale wadogo, hakika, na kondoo ni wale wazima. Kwa hivyo wote wadogo kwa wakubwa, lisha kundi la kondoo wa Mungu! Ona? Na Lilishe kwa Neno! Lile Neno (mwaona) ni Kweli! Yesu alisema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu." Sivyo? Kwa hivyo basi, kama mtu ataishi nao ni kundi la Mungu, hii—kanisa, ndipo watasitawi kwa Neno na Mana ya Mungu. Hii ni Mana Yake!

83 Katika Bi—Biblia, ndiyo kwanza tuyapitie pale katika zile—katika zile—katika zile Nyakati za Kanisa. Yesu ndiyo ile Mana iliyofichwa; Kristo ndiye Mana ya kanisa. Mana ni nini? Mana katika Agano la Kale ilikuwa kile kilichoshuka upya toka Mbinguni kila usiku kupea kanisa nguvu katika safari yake. Sivyo? Sasa, katika Agano Jipya ile Mana iliyofichwa ni nini? "Kitambo kidogo na ulimwegu haunioni tena (imefichika); bali ninyi mtaniona, maana nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Na Kristo ndiye Mana iliyofichwa itokayo kwa Mungu Mbinguni upya kila siku—kila siku.

84 Hatuwezi kusema, "Vema, majuma mawili yaliyopita nilikuwa na ujuzi mkuu wa Mungu." Na sasa hivi je? Ona? Kila siku, mpya, baraka mpya, kitu fulani kipya kikija toka kwa Mungu, ile Mana iliyofichwa ikishuka toka kwa Mungu Mbinguni, Kristo. Na tunaila Mana hii ambayo ni Kristo, na Yeye hutupea nguvu safarini kote hata tutakapofika ile—ile nchi kule ng'ambo.

85 Sasa, hayo ndiyo Yeye alimaanisha kwa, "Lisha kondoo Zangu." Kama tungaliingilia hayo, hatungelifikia mengine yaliyosalia, kwa sababu hilo ni zuri sana kwangu. Napenda hilo, ninaponena kuhusu Kristo kuwa Mana na Chakula cha kondoo.

86 Walishe Kristo kwa Neno Lake. Ona? Chukua Neno la Kristo jinsi hasa limeandikwa hapa ukawape kondoo. Haijalishi yale mtu ye yote asemayo, "Ee, wanahitaji andazi!" Usiamini hilo. Hilo ndilo wanalohitaji, hapa! Ndilo hilo Ona? Wape Hili! Hili ndilo Chakula cha Kondoo. Hicho ndicho kinachowafanya wakue. Yule Roho Mtakatifu, hili ndilo Neno Lake, agizo Lake. Neno ni Mbegu. Mbegu huzaa mmea; tunaokula. Sasa, hiki ndicho kinachokuza ule mmea ambao Roho Mtakatifu husitawi kwake, ni kanisa. Linakula . . . Ana—ana—analisha Kanisa, Roho Mtakatifu hufanya hivyo, akifurahia katika uwepo wa Mungu, kwa sababu watu wanaamini Neno Lake na kumruhusu Yeye afanye kazi kwao, akiwapa vitu vile vile ambavyo Mungu aliwaahidi wao kuwa watavifanya. Na Mungu anaona Kanisa Lake likistawi kwa hivyo kondoo wanalishwa, na Roho Mtakatifu akitukuzwa. Ona? Naam. "Lisheni kondoo Zangu!" Vema.

Sasa, kama haya hayatoshi, basi mnijulishe baadaye.

**154. Ndugu Branham, nilipopitia katika ule mstari wa maombi muda mfupi uliopita, niliwekewa mikono yenye upako na maombi yakafanywa kwa ajili ya mume wangu ambaye hajaokoka bado. Nilijawa na nguvu za Bwana! Je, hii ni ishara dhahiri kuwa yeye ataokoka?**

87 Vema, . . . Haikosi kuwa ni mwanamke, Dada, singe—singedhani hiyo ilikuwa ishara dhahiri kuwa mumeo ataokoka, ingawa naamini kama—kuwa Mungu, ili- . . . Naamini yeye ataokoka, bila shaka, lakini kusema . . . "Sasa, ungesema hilo ni BWANA ASEMA HIVI?" Jihadhari na hilo (ona?), kwa sababu, ona, huenda ikawa ni baraka za Roho Mtakatifu juu yake, kwa sababu umechukua msimamo wako kwa Kristo. Ona?

88 Unakuja hapa na kusimama kwa niaba ya mumeo mwenye dhambi kama Kristo alivyoenda msalabani kwa niaba ya kanisa lenye dhambi. Waona? Ulifanya jambo kuu. Lakini kile ningefanya . . . Kama upo asubuhi hii, kama wewe uliyeandika swali hili, kile ningefanya, ningeamini kwa moyo wangu wote kuwa Mungu atalitenda (ona?)—kuwa Mungu atalitimiza, kwa sababu au Yeye alikupea baraka au Yeye hakukupea, hicho kilikuwa kitu kingine zaidi ambacho Mungu alikupea. Lakini naamini ingeku—ingekufanya ujisikie vizuri, kwa sababu Yeye alikubariki.

89 Ni kama tu kama ungelinena kwa lugha, na hakuna mfasiri kanisani, naam, haikupasi kunena kanisani isipokuwa kuna mtu wa kufasiri lugha hizo. Lakini ukinena kwa lugha, na hakuna mwenye kufasiri . . . Basi, tumia . . . wewe . . . Po pote

mlipo katika maombi, manyumbani mwenu au ko kote mliko, nena basi, kwa sababu, "Yeye anenaye kwa lugha zisizojulikana hujijenga mwenyewe." Inampa faraja. Ona? Yeye ajisikia vizuri, kwa sababu yeye yuasimama pale akiomba na muda si muda, Roho Mtakatifu anamjia mwanamume yule au mwanamke yule nao wanaanza kunena kwa lugha. Na nafsi zao zilikuwa zikifurahi na changamfu, kwa sababu wao—wao walinena kwa furaha. Ona?

90 Naam basi, hiyo ilikuwa—hiyo ilikuwa—haikuwa ishara tu kuwa Mungu angejibu maombi uliyokuwa ukiomba, bali ilikuwa ishara kuwa Roho Mtakatifu anakusikia. Ni—ni . . . Yeye akujua; Yeye yu pamoja nawe. Ningetumia jambo lilo hilo kwa hili. Roho Mtakatifu akikupea wewe ba—baraka.

91 Hapa wakati mfupi uliopita. Wakati wa mwisho niliponena kwa lugha, kama ninavyoweza kukumbuka, ilikuwa . . . nilikuwa . . . Imekuwa yapata miaka mitatu au minne iliyopita. Ilikuwa kule Illinois, na Billy alikuja kuniita kwa—kuenda kwa—kwa ajili ya mstari wa maombi kule Zion City. Nami nilikuwa na mzigo moyoni mwangu, nami nikapiga magoti na kuanza kuomba. Na nilipokuwa nikiomba, nili—nilimsikia Billy akija na kubisha mlangoni. Nami nikasema, "Billy si—siwezi kuenda sasa." Naye alienda nje kule akaketi.

92 Nami nilikuwa nikiomba, moyo wangu ukiwa mzito; si—singeenda kanisani hivyo. Na tazama, mara nyingi wakati mwingine Yeye hunipa ono kunionyesha kitu fulani kitatendeka, lakini Yeye hakufanya hivyo wakati huo. Nami nilikuwa nikiomba chumbani mle, nami nikamsikia mtu fulani akinena. Nikaacha kuomba. Nikasikiza, na kuna mtu fulani mlangoni, walikuwa . . . Ilionekana kama lugha ya kigeni, kama Kijerumani au Low Dutch, ama cho chote kile; ilikuwa upesi sana, kutatarika. Nikasikiza tena, nami nilidhani, "Vema, mtu fulani amekuja pale na anaongea na mwenye mkahawa katika Kijerumani; labda yeye atamjibu."

93 Nami nikaacha kuomba, nikaegemea kitini nikisikiza, naye akaendelea tu kunena. Nikawaza, "Vema, nashangaa mbona hamna mtu anayejibu." Nami nilisikiza; nikawaza, "Vema sasa, si ajabu hiyo."

94 Kulikuwa na mizani kule barabarani nami nilisikia mtu yule kule chini akipaza sauti, "Endesha!" mwajua, na "Endesha!" Nikageuka, nikatazama upande ule, na nilipofanya vile, nikajisikia . . . nikatambua, mimi ndimi niliyekuwa nikinena. Ndimi. Nami nikanyamaza kimya kabisa bila kujua kitu kimoja. Sikuwa na mamlaka kamwe juu ya yale niliyokuwa nikinena, sikujua jambo lo lote nililokuwa nasema, hata moja. Mimi tu . . . Kinywa changu kilikuwa kikipanuka-panuka, nami nilikuwa nikinena lugha fulani. Nilitulia kabisa. Baadaye ikaniondokea. Na iliponiondokea lo, jamani, nilijisikia kama ningepaza sauti,

mimi tu—mwenye furaha tele. Sijui kwa nini, lakini uzito wote uliniondokea.

95 Kwa hivyo nilienda kanisani wakati huo, nikamwita Billy. Na nilipofika kanisani. . .Bw. Baxter wakati ule alikuwa msimamizi wa mkutano. Naye alikuwa akiimba, akingoja. Nilikuwa nimechelewa kwa zaidi ya nusu saa. Na nikamwambia nilikuwa tu nimechelewa.

Na—naye akajua nilikuwa nikilia, naye alisema, "Kuna nini?"

96 Nami nilisema, "Si kitu." Nami nikaendelea na baada ya kama dakika kumi hivi, mwanamke akaingilia upande wa nyuma wa ule ukumbi, naye alikuwa karibu kupata nafasi kule nyuma. Na tulipochunguza mwanamke yule, tupate kujua, alikuwa safarini kutoka Twin Cities (St. Paul na Minneapolis, mahali fulani, mojawapo wa miji hiyo), ile. . .Alikuwa hajiwezi kwa ugonjwa wa kifua kikuu kwenye—ile motokaa ya kubebea wagonjwa haingedhubutu kumleta, mapafu yake yalikuwa magonjwa sana, mororo tu. Na kwa hivyo ndugu kadha walichukua motokaa kuukuu ya Chevrolet, na kuondosha kiti cha nyuma, na kuweka machela ndani humo kwa njia fulani, ama kitanda, wakamlaza juu yake, nao walikuwa wakimleta mkutanoni. Yeye alitaka kuja.

97 Madaktari walikuwa wamemkatia tamaa. Nao walipokuwa wakija. . .Walimwambia mtikiso mdogo tu, angeanza kutokwa na damu, na ikawa hivyo. Naye akaanza kutokwa na damu. Nao iliwapasa wamwondoe nje na kumtandaza nyasini. Na watakatifu walikuwa wamesimama pale wakimwombea mwanamke yule. Naye alikuwa tu. . .Kila alipopumua, ililia guruguru tu, damu ingetokea kinywani mwake, hivyo.

98 Kwa ghafula, akaponywa papo hapo! Naye aliruka juu toka pale na akaanza kufurahi, akaja kanisani. Ndiye huyo kule nyuma akitoa ushuhuda, kule nyuma.

99 Nilisema, "Ulikuwa wakati gani?" Naye alipotaja wakati, ilikuwa wakati gani, ulikuwa wakati ule ule ambao kunena kule kulikuwa kunaendelea kupitia kwangu. Vema, ilikuwa nini? Ilikuwa ni Roho Mtakatifu akiomba kwa ajili ya mwanamke huyo pale! Mwafahamu ninalokusudia?

100 Sasa, Biblia inasema hayo. Wakati mwingine sisi hugugumiza maneno; hatujui yale tunayonena. Lakini ni Roho Mtakatifu ndani mle akijitokeza, akiombea mambo tusiyoyafahamu. Ona?

101 Na mwanamke yule aliponywa papo hapo. Tulisikia toka kwake kwa muda mrefu toka pale. Yeye ni mzima kabisa, alipona.

102 Sasa, mwaona, Mungu ajua pale mambo hayo yaliko, na Yeye ana njia ya kuyafanya. Ona? Yeye ana njia Yake Mwenyewe

ya kuyafanya. Yatupasa tu tujitolee wenyewe kwa yale Yeye anayofanya. Ndiposa—basi jambo gumu kufanya basi unapofika pale ni kujishikilia katika ile ncha ya upanga iliyomo kati ya ushupavu wa dini na Ukweli.

103 Sasa, usipochunga, shetani atakutupa katika kundi la wazushi na utapoteza ujuzi wako wote, na mengine yote. Ona? Unapofanya hayo, lakini ukiweza kushikilia Kweli imara, utazame Biblia, na ukae nayo, na uwe mpole na mnyenyekevu, Mungu atazidi tu kukupeleka kuelekea Kalvari, kuendelea safarini hivyo, kama utakaa na hilo.

104 Na hicho ni kitu kama chako kilivyokuwa, Dada. Mungu alikuwa tu akikupea baraka. Huenda ikawa ushuhuda halisi kuwa wewe uta-. . .Lakini singetegemea hayo (mwaona?), kusema, "Bwana aliniambia!" sababu ya kueleza tukio hilo ni kwa kuwa huenda likakutia moyo kuendelea kuamini. Cho chote ambacho Mungu alitenda pale, kuleta Roho juu yako hivyo, ilikuwa kwa kusudi fulani. Huenda ilikuwa kitu kinginecho; bali kama ilikuwa kwa ajili ya yeye bila shaka ataingia moja kwa moja katika ufalme wa Mungu. Naamini hilo.

**155. Ndugu Branham, si ni kulingana na Maandiko wanawake hapaswi kunena Kanisani?**

105 Yeye ana maswali mawili hapa. Hiyo ni kweli. Ni—ni kweli. Ni—ni kweli. Si halali kwa wanawake kuwa wahudumu na—na kunena kanisani. Hiyo ni kweli, I Wakorintho sura ya 14.

106 Hakika kanisa lote hapa, nyote mwajua hili. Na huyu huenda ni mgeni ndani humu asubuhi hii, sijui. Lakini si halali kwa—kwa wanawake ku—kuwa—kuhudumu. Hilo—hilo ni kweli.

Nitaisoma tu kwenu hapa, na—nanyi mtaona. Ndiposa mta—mtajua. I Wakorintho sura ya 14 naamini. Nitaipata tu kwa dakika moja, nikiweza kupapata . . . Naam, hii hapa.

> *Wanawake na wanyamaze katika kanisa, maana hawana ruhusa kunena; bali watii kama inenavyo torati.* (Sasa, torati haikuwaruhusu wanawake kuwa makuhani na kadhalika katika siku zilizopita. Ona?)
>
> *Nao wakitaka kujifunza neno lo lote, na wawaulize waume zao wenyewe nyumbani mwao; maana ni aibu wanawake kunena katika kanisa*

107 Sasa, mkiangalia Korintho hapa . . . Wengi wa hawa Wakristo wa Korintho na wengi wa . . . Yule mungu mkuu wa kike ulimwenguni katika siku hizo alikuwa Diana, ambaye alikuwa mungu wa kike wa Warumi. Naye alikuwa mungu wa kike wa Efeso. Naye aliabudiwa kote ulimwenguni. Na sasa, wahudumu wake . . . Bila shaka, kwa kuwa yeye alikuwa mwanamke, basi hilo liliwafanya wahudumu wake wanawake. Na walipoongoka kuwa Wakristo kupitia kwa Paulo . . . Sasa,

Paulo alikuwa gerezani ambapo yeye aliandika nyaraka hizo, bila shaka, kule Rumi.

108 Sasa, wao walimwandikia yeye barua, mwaona, baada ya kuanza kunena kwa lugha na karama kuu zilipoanza kufanya kazi kati yao. Vema, wanawake hawa walidhani wangeendelea na huduma yao.

109 Sasa, mkichunguza, ninyi mnaosoma Biblia zenu, kile kifungu cha 36 yeye alisema.

> *Au je! Neno la Mungu lilitoka kwenu? au kuwafikia ninyi peke yenu?*
>
> *Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*
>
> *Lakini . . . mtu akiwa mjinga na awe mjinga.*

110 Sasa, vinginevyo, wanawake . . . Sasa, kama utachukua historia ya waraka huu (ona?), wa kanisa hili, wanawake hawa walidhani walikuwa . . . wangeendelea na huduma yao kama kwamba wao walikuwa ma—makuhani wa Diana, yule mungu wa kike. Mungu si mwanamke; Mungu ni Mwanamume. Na kuna mmoja tu aliye halisi, na huyo ni mwanamume. Mwanamke ni kitu kilichotoka kwa mwanamume. Mwanamume hakuumbwa kwa ajili ya mwanamke, ila mwanamke aliumbwa kwa ajili ya mwanamume. Ona? Kama ungefungua tu kufahamu kwako kwa kiroho. Ninyi, mwaona? Mwaona?

111 Mwanadamu—mwanadamu alipokuja duniani kwanza, yeye alikuwa mwanamume na mwanamke pia, wa kike na wa kiume kabla yeye hajawa na jinsia. Ona? Roho wa kike, ile roho ya chini zaidi, ndiyo iliyo oga. Ndiposa kunayo ile jasiri, mwanamume. Lakini Yeye alipomfanya na kumweka mbalimbali . . . Ili azaane ulimwenguni, Yeye aliondoa roho ya kike kwake na akaondoa ubavu mmoja toka mbavuni mwake akamfanya mwanamke.

112 Mwanamke hakupaswa kuwa mtawala! Yeye alipoanza hayo kwanza, alisababisha uzao wote wa mwanadamu kuanguka. Ona? Ee, na hata ilikuwa . . . Yeye alikuwa chanzo cha kule kuanguka. Ndiposa Mungu akamwinua na kuleta uzima tena ulimwenguni kwa Kristo kupitia kwa mwanamke. Bali hamna mahali po pote ambapo mwanamke aliruhusiwa ku—kuwa mhudumu katika kanisa.

113 Katika 2 Timotheo sura ya 3, yeye alisema, "Simpi mwanamke ruhusa ya kufundisha, wala kumtawala mwanamume, bali awe katika utulivu." Mwaona? Na si sahihi kwa mwanamke kuhubiri; hilo ni kweli.

114 Sasa, najua nimewaona wanawake waliokuwa wahubiri kweli kweli—wangehubiri pia—kama Aimee McPherson na wengi wa wanawake hao pale. Lakini weka mkono wako juu yao kwa muda mchache. Ona? Si . . . Najua watu ambao wangeweza

kunena kwa lugha asubuhi hii wanaoketi papa hapa katika kanisa hili. Kusingelikuweko wenye kufasiri, hawangethubutu kufanya hivyo. Ona?

115 Yawapasa mkumbuke ya kwamba hao wanawake walizaliwa chini ya ukoo fulani, kusudi wao . . . Kuzaliwa kwako kuna uhusiano mwingi nako. Ni jina lako, vyako—yote yanayokuhusu wewe (mwaona?) yana uhusiano nayo, haijalishi ni nini.

116 Ningeondoka nje hapa na kufyatua risasi na kumwua mtu asubuhi hii, lakini singethubutu kufanya hivyo. Lakini naweza kufanya hilo, hakika. Ona, ningemwua mtu kama tu vile ungemwua kuchakulo; lakini hu—hupaswi kutenda hilo. Ona? Na hilo ni jambo lile lile. Yakupasa uchunge mambo hayo, sasa kwa kuwa hufanyi . . . Hizi ni amri za Bwana.

117 Walipoyaandika tena na kusema, "Naam, Roho Mtakatifu alitwambia!" (ona?), Paulo alisema, "Au je? Neno la Mungu lilitoka kwenu? Au je, lilitoka kwenu peke yenu? Kama mmoja wenu nyote—kama mna manabii wote kule, watayatambua kuwa hayo ninayosema ni maagizo ya Bwana. (Ona? Naam!) Lakini kama kunaye mtu ye yote aonyeshaye kwa—kwa—kwamba yeye anataka kutenda kinyume, akitaka kuwa mjinga, na awe mjinga. (Ona?) Mwache peke yake na aendelee. (Ona?) Usifanye lo lote kinyume cha hayo." Lakini kumbukeni, mwanamke hapaswi kunena katika kanisa.

118 Na kwa hivyo, hapo ndipo ambapo unaweza kuamua kama mchungaji wako au cho chote kile, kama yeye yu wa rohoni au la. Ona? Yeye alisema, "Mtu akijiona kuwa ni mtu wa rohoni au nabii, na ayatambue hayo ninayonena ya kwamba ni maagizo ya Bwana." Ona?

119 Hiyo ndiyo sababu nawaagiza watu wabatizwe tena katika Jina la Yesu Kristo. Paulo alifanya hivyo, naye alisema, "Ijapokuwa malaika wa Mbinguni atawahubiri ninyi kitu kingine, isipokuwa hiyo, na alaaniwe." Na ndiyo ile imekwisha fundishwa hapa pia. Mtu ye yote akija . . . Kama malaika akitoka mbinguni na kusema "Wanawake na wahubiri, watawazeni wawe wahudumu!" Biblia ilisema, "Na alaaniwe." Hili ni agizo la Bwana hapa.

**156. Lo, ni sawa kwa mwanamume Mkristo na mwanamke Mkristo kubusiana wao kwa wao (Ee!) wanaposalimiana?**

120 La, bwana! Hasha! La, bwana! Unambusu mwanamke mmoja, ndugu, na huyo ni mke wako (ona?), au mtoto wa—wako, au . . . Ona?

"Je, ni sawa kwa . . . " Hebu nione kama nilipata hilo sahihi! "Je, ni haki kwa mwanamke Mkristo kubusiana wao kwa wao wanaposalimiana?"

121 La bwana! Hasha! Hiyo . . . Msithubutu kamwe kuanzisha hayo! Naam, bwana! La, bwana! Kaeni mbali na wanawake! Waondokeeni! Naam!

122 Sasa, wao ni dada zetu, lakini msi- . . . Sasa, wana hilo. Kuwa katika . . . Jambo lile hata liliingia katika Pentekoste, na linaitwa "upendo huru." Na unapofanya—unapopata cho chote kama hicho, kiondokee. Naam!

123 Sijali u mwadilifu vipi . . . Wewe ni ndugu yangu, na—nami naamini kuwa una—huenda u mwanamume mzuri aliyetakaswa na mtakatifu. Sijali u mtakatifu vipi; wewe bado u mwanamume. Nami sijali mwanamke yule ni mtakatifu vipi; yeye bado yu mwanamke. Acheni hayo hata mtakapooana. Fanyeni hivyo tu!

124 Kumbuka, mwili huu . . . Nitazungumza viwili ili ninyi watu mfahamu. Ni kundi lililochanganyika, lakini mimi ni ndugu yenu, na hili ni swali. Ona?

125 Kila mwanadamu mwanamume kwa mwanamke wana namna ya vifuko mwilini vinavyotofautiana. Mwanamke ana kifuko cha kike, vifuko vya jinsia. Mwanamume ana vifuko vya kiume, vifuko vya jinsia. Na vifuko hivyo vimo kinywani mwa mwanadamu. Naam.

126 Na hapa kuna kitu kingine ambacho huenda kikazushwa, mwanamume kumbusu mwanamume mwingine mdomoni. Hilo ni chafu! Hilo ni ovu! Na lafanyaje? Laanzisha ulawiti. Liondokee hilo! Mwasema . . .

127 Mtu fulani aliniuliza si muda mrefu umepita, kasema, "Ndugu Branham, naam, walisalimiana kwa busu takatifu." Walibusiana nyuma kwa shingo, walishikana shingo kwa shingo, na kubusiana nyuma ya shingo. Hiyo ilikuwa kabla ya kuanzishwa kusalimiana kwa mikono. Ni salamu. Hivyo ndivyo ilivyo. Hawakusalimiana kwa mikono; walikumbatiana wao kwa wao na kubusiana nyuma ya shingo, si kinywani, usoni. Hilo husababisha upotovu. Liondokeeni! Msithubutu kamwe kufanya hivyo!

128 Siku hizi sisi husalimiana kwa mikono sisi kwa sisi. Mkitaka . . . Unamkumbatia ndugu yako, na kumbusu shingoni, au yeye anakubusu shingoni, hilo ni sawa. Lakini usimbusu mwanamke huyo, na usimkubalie mwanamke huyo akubusu. Ona? Naam! Mshike kwa mkono pale, umwambie, "Ngoja kidogo, Dada, hebu kidogo hapa (ona?); hebu tuelewane!" Na kwa hivyo, sasa fanyeni vile.

129 Sasa niliwaambiaje muda mchache uliopita nilipoanza? Unapoona cho chote—motokaa ikija njiani kwa mwendo wa maili tisini kwa saa, iondokee. Naam! Uonapo upotoe wa kwanza katika lo lote kama hilo, liondokee; uondokee! Kisha . . . Haupaswi kuwa mahali hapo. Shetani atakuletea jambo ambalo litakaloangamiza nafsi yako na kukupeleka kuzimuni. Liondokee! Jitenge na ubaya wa kila namna. Naam!

130 Uwe mwanamume, uwe mwanamke, kama . . . Nitawashindania wanawake kidogo. Hilo si la kawaida, sivyo? Wao—wao husema, “Ee, mwanamke aliisababisha! Ee, makosa yalikuwa ya mwanamke. Kama hangeondoka mahali pake, vema, mwanamume hangeondoka pake.” Hiyo ni kweli. Hilo—tutasema hilo ni kweli. Yeye huondoka mahali pake. Mwanamume hawezi kuwa mbaya isipokuwa kuweko na mwanamke mbaya; lakini kumbuka hakuwezi kuwa na mwanamke mbaya isipokuwa kuwepo mwanamume mbaya. Naam!

131 Nanyi mnaodai kuwa wana wa Mungu, msimamo wenu uko wapi? Kama mwanamke hayuko katika mahali pake, si wewe u mwana wa Mungu? Je, si wewe ndiwe uliye bora, na chombo chenye nguvu? Kama Biblia isemavyo yeye ni mdhaifu zaidi, ndipo kama yeye yu chombo kidhaifu, basi jionyeshe mwenyewe mtu wa Mungu. Mwambie, useme, “Dada, umekosea.” Hiyo ni kweli! Nimefanya hilo, na Wakristo wengine wamefanya hilo. Na utafanya hivyo mradi tu wewe ni Mkristo, lakini jitambulishe mwenyewe. Wewe u mwana wa Mungu. Wewe u—una nguvu zaidi juu ya nafsi yako kuliko mwanamke alivyo. Kama yeye yu dhaifu, mtambue yeye kuwa mdhaifu. Fahamu makosa yake, na mambo kama hayo au jaribu kumsahihisha mwanamke huyo. Sema, “Dada, sisi ni Wakristo, haitupaswi kufanya hayo.” Ona? Kuwa mwanamume halisi, kuwa mwana wa Mungu ukawachunge wanawake hao.

132 Na hapo ndipo kule kuanguka kukuu kulipoanza hapo mwanzo. Ilikuwa Shetani na Hawa. Hilo ndilo lililosababisha kuanguka kwote kwa uzao wa mwanadamu ni kupitia hayo.

133 Na kama wewe ni mwana wa Mungu, kuwa na nguvu; kuwa mwanamune thabiti. Kama hauko hivyo, kaa madhabahuni hata uwe hivyo. Basi jitengeni na ubaya wa kila namna. Na msianze sasa kusalimiana . . .

134 Mtu fulani aliniambia wakati fulani uliopita ya kwamba waliyaona hayo mara mbili au tatu kanisani mwangu hapa, ya . . . Si hapa kanisani, lakini watu wajao kanisani. Na kama mgeliketi hapa asubuhi hii, ningewachimbulia hili vizuri sana. Ona?

135 Wanawake, wasichana, wakija na wanaume hawa wakiwabusu wanawake hawa. Msithubutu kufanya hivyo! Usi- . . . Jitengeni nayo. Ewe, kumkuka hilo! Ikiwa yeye ni kijana mwanamke, hajaolewa, au cho chote kile; yeye atakuwa mke wa mtu fulani siku moja. Nawe haikupasi kufanya hayo. Jitenge nayo. Ukitaka kumsalimia, basi kuwa mwana wa Mungu, salimiana naye kwa mkono na kusema, “Washindaje, Dada.” Na hiyo iishie papo hapo. Ona?

136 Jitenge na mambo hayo; ni machafu. Na punde yatakuingiza shidani. Basi . . . Ee, hilo . . . Dhambi ni rahisi sana, na inavutia

mno, na ya inapendeza mno. Ni rahisi kuanguka kwake. Jambo bora kufanya ni hata kule kuonekana kwake, kuondokee! Rudi nyuma! Uwe Mkristo halisi!

137 Na kwa wanaume kubusiana, ukimbusu ndugu yako shingoni, na uantaka kulifanya, hilo ni sahihi. Usimbusu mwanamume ye yote kinywani, na mdomoni, au lo lote kama hilo, kwa sababu hilo—hilo si sahihi. Ona? La, hilo—hilo laonyesha kuna kitu fulani kidogo kasoro tangu mwanzo. Ona? Kwa hivyo ondoka pale, kataa hayo. Msi—msianzishe hayo maskanini hapa. La, sisi hakika hatutastahimili hayo kwa vyo vyote vile. Ona?

138 Wewe—kama ukitaka kumwona ndugu yako, ukitaka kumbusu shingoni, vema, endelea ukafanye hivyo, lakini usiwabusu watu midomoni, kwa sababu hilo haliwezekani; hilo si sahihi! Huanzisha tu upotovu. Huanzisha ulawiti na mengineyo.

139 Na kuna mambo wawili pekee yatakayotendeka katika mambo hayo hivyo . . . Mkianza . . . Acha wanaume . . . niliona . . . Ee, wakati mwingi kati ya watu, watakuja. Nimeona makanisani, na mhuburi angeingia, akamwendea na kumshika kwa ghafula kila dada, na kumkumbatia na kumbusu na kumketisha chini. "Washindaje, Dada, Haleluya!" Anaunyosha mkono na kumshika huyu na kumbusu. Anaenda kote kanisani hivyo. Kwangu hilo ni kosa!

140 Nilipokuwa kule Finland, sote tulikuwa pale . . . Huenda mmejua hili, tulikuwa na mikutano, nami nilikuwa kule kwa Y.M.C.A. Hakukuwa na sabuni, wala sabuni ya unga nchini Finland. Na kitu pekee . . . Nilikuwa na sabuni ya kunyolea, na kila mmoja wetu ilimpasa kusimama na kuoga kidogo tu, mwajua, na hii sabuni ya kunyolea. Tulikuwa tu na kipande kimoja pekee, na hakukuwa na sabuni katika Finland. Nao walioga tu kwa kitu fulani, na karibu kiondoe ngozi yako.

141 Kwa hivyo basi sisi . . . Walitwambia watatupeleka atika mavusho ya Kifini. Na tukaenda kule kwa Y.C.A. Tukaenda kule kuoga. Hayo ni ya Kifini, yale mavusho mashuhuri sana ya Kifini. Na nilikuwa nimeshaoga huku hapo mbeleni, kulikuwa kuzuri. Niliwaza "Vema, tunaenda ku- . . . Ni Y.M.C.A. Kwa hivyo itakuwa vema."

142 Lakini nilipoanza kuenda kule, Roho Mtakatifu akaniambia, "Usifanye hilo. (Lo, ni vizuri sana kuwa na Roho Mtakatifu.) Usifanye hivyo."

Vema, nilisema tu papo hapo, nikasema, "Siamini nataka kuoga asubuhi hii."

Daktari Manninen na wengineo wakasema, "Ee, Ndugu Branham," kasema, "Lo, kuna vyumba vikubwa vya vioo!" na kasema, "Ni mazuri." Kasema, "Si . . . "

Kwa kawaida kile wafanyacho, wanamwaga maji kwenye mawe haya na kukujaza mvuke, kisha wanakupigapiga kwa majani ya mti hivyo, ndiposa—ndiposa unakimbia na kujitumbukiza katika maji baridi. Hao Wafini huenda katika theluji na barafu na vitu kama hivyo. Bali, bila shaka, wao wamehudhuria hayo; watu wakubwa mno na wanene. Nao wanarudi, na kuoga kwenye mavusho haya yenye joto, yenye joto kisha kwa ya baridi, upesi hivyo. Bali waliniacha nisimame palipokuwa na hewa yenye baridi, kisha nikarudi, maana singefanya hivyo. Niliogopa moyo wako usije ukazimia, kwa kufanya hivyo, na sikuwa nimezoea hayo.

Kwa hivyo ni—niliyapenda sana, bali Kitu fulani kikaniambia nisioge kule. Vema, Ndugu yangu Howard, na Ndugu Baxter, na hao wote wakienda kule, na wandugu, hao wengine wote, mwajua, wote wakizungunza, mwajua, wakienda kule. Kwa hivyo nikajisikia vibaya, mwajua, kwa sababu Roho Mtakatifu alisema, "Usifanye hivyo."

Kwa hivyo tukaenda kwa Y.M.C.A., nao wakaja, hao wote pale wakinisalimia. Kisha, lo wao wa—waliandika vichwa vya maneno katika magazeti, ukurasa wa kwanza na wa pili kila siku, ile mikutano. Nao walikuwa huko.

Nikaingia katika chumba kidogo nikaketi chini, nao wote wakaingia chumbani kutoa nguo. Hao walipokuwa mle waki- . . . kutoa nguo, huyu msichana mdogo anakuja, mrembo, hapa mwenye nywele ya shaba; wao ni watu wazuri, ni wasafi, watu waadilifu wawezavyo kuwa. Ndiye huyu hapa nnakuja, taweli mgongoni mwake, akaanza kuingia mle chumbani. Nikasema, "We, we, we! Usiingie! Shshsh!" Nikajaribu kumsimamisha. Akageuka akacheka, akaenda zake ndani.

[Mahali patupu—Mh.] ". . . wanawake kusugua, Ndugu Branham."

Nikasema, "Sijali wao ni nini. Ni kosa. Si haki." Nikasema, "Na maumbile yenyewe yawafundisha."

Yeye akasema, "Hasha, Ndugu Branham, wao wamekuzwa tangu utotoni, kusuguana. Ni kama tu wauguzi wenu Amerika, mambo kama hayo, wao wamekuzwa hivyo."

Nikasema, "Sijali wao ni nini, hilo bado ni kosa. Kabisa. Ni wanaume na wanawake, nao wanapaswa kutenganishwa na kuvalia nguo mahali mbalimbali." Amina.

Sitaki kuanzia hayo, nitahubiri haya baadaye, sivyo? Vema.

**156. b. Eleza Imani ya kimitume.**

Hilo ni swali moja. Kuna maswali moja, mbili, tatu. *Imani ya Kimitume* maana yake ni "ile imani ya mitume." Hiyo ndiyo maana ya imani ya kimitume, ya kwamba udumu katika Biblia. Sasa ile inayoitwa imani ya kimitume siku hizi, wengi wao

hawadumu na Biblia. Bali kimitume maana yake ni—ni Imani ya kimitume, Imani ya Kimitume ya Biblia. Vema.

**156. c. . . .na kundi linalojiita la kimsingi, je makundi haya mawili yameokolewa?**

Sasa, sijui. Ona, singelijua jinsi ya kulijibu hilo. Sasa, "Je, haya makundi yameokolewa?" Sijui.

**Eleza tofauti kati ya roho na . . .**

Vema, ni swali tofauti sasa.

Sasa, "Je, makundi haya mawili wameokolewa?" Hebu tulifanye dhahiri sana kwako, na kusema, "Sijui. Singejua."

Sasa kumbuka, mawazo yangu ndiyo haya, huenda yasiwe sahihi. Mawazo yangu ni kwamba, kama Mkatoliki wa Kirumi, ama yo yote yule, Mmethodisti, Mpresbeteria, mfuasi wa kanisa la Kristo, Mlutheri, ye yote yule, iwapo anamwamini Bwana Yesu Kristo na anamtumainia kabisa kwa wokovu wake, naamini ameokolewa.

Bali, unaona, Kanisa Katoliki la Kirumi halifanyi hivyo. Wao wanaamini ya kwamba kanisa huwaokoa. Ona? Wo—wokovu wao umo kanisani. Kama huyu kasisi alivyokatazwa kububiri radioni, hapa wakati mchache uliopita, kwa kusema, "Hakuna wokovu mwingine, isipokuwa tu katika kanisa, ona, kanisa la Kirumi." Sasa, hilo ni kosa. Wokovu uko katika Yesu Kristo. Hiyo ni kweli. Si katika kanisa, bali katika Kristo.

Sasa kama yeye ni wa kimitume, ama, wa kimitume na wa kiasili siku hizi hujiita . . .

Naam, ni kama wa kiasili alivyonijia, hapa wakati mfupi uliopita, naye akaniambia, akasema, "Yaonekana unaegemea Ukalvini, sivyo?"

Nikasema, "Vema, mradi tu Mkalvini anadumu katika Biblia, niko pamoja naye." Nilisema, "Ninaingia tu katika Biblia, na iwapo Kalvini anadumu katika Biblia. Bali akitoka katika Biblia, basi mimi nitaendelea tu, niamini Biblia."

Yeye akasema, "Vema," akasema, "nataka kukwambia jambo fulani. Ulisema, nimekusikia ukisema ya kwamba mtu akiisha kuokolewa, ya kwamba hangalipotea kamwe."

Nikasema, "Hivyo ndivyo Maandiko yanavyosema hasa. Tuna Uzima wa Milele, naye hataingia katika lawama ama . . . hukumu, bali amepita toka mautini kuingia Uzimani." Nilisema, "Mimi . . . Si mimi niliyesema hayo, huyo alikuwa ni Yesu Kristo aliyesema hayo."

Yeye akasema, "Nataka kukuuliza kitu fulani basi," kasema, "Je, unaamini Sauli alikuwa ameokoka?"

Nikasema, "Yule Sauli, yu—yule mfalme Sauli?"

Akasema, "Naam."

143 "Naam," nikasema, "Hakika!"

Alisema, "Sasa kumbuka, yeye alikuwa nabii."

144 Nilisema, "Bila shaka, Biblia ilisema yeye alitoa unabii pamoja na manabii. (Yeye alikuwa na karama ya unabii. Yeye hakuwa nabii, bali alikuwa na karama ya unabii, kwa sababu yeye alikuwa huko chini pamoja na wale manabii walipokuwa wakitoa unabii." Lakini twajua kuwa Samweli ndiye aliyekuwa nabii katika siku hizo, kwa hivyo . . .) Lakini Sauli alikuwa akitabiri pamoja na manabii."

Yeye alisema, "Basi kama yeye alikuwa nabii, basi alikuwa ameokoka?"

Nikasema, "Kabisa!"

Yeye akasema, "Basi nataka kukuuliza jambo fulani." Kasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani." Kasema, "Ndiposa unasema Sauli aliokoka, na yeye—Biblia ilisema kuwa Bwana alimwondokea naye akawa adui wa Mungu, kisha akajiva, halafu wasema kwamba yeye aliokoka?"

145 Nilisema, "Na wewe u mwamini wa kiasili?" Nikasema, "Ndugu, ndugu, wewe huisomi sahihi, hivyo tu. Hausomi vile Maandiko yanavyosema."

Yeye akasema, "Vema, Sauli hangeokolewa kama yeye alikuwa adui wa Mungu."

Nikasema, "Sauli aliokoka."

"Jamani!" Yeye akasema . . .

146 Nikasema "Yeye alikuwa nabii, hapana budi alikuwa ameokoka. Ona? Mungu alimwokoa, na Mungu si mtoaji wa Kihindi, kama tusemavyo. Yeye ha- . . . Vema, kama Mungu akikupea Roho Mtakatifu akijua Yeye atakupoteza papa hapa chini, basi, hilo lingekuwa jambo la kipumbavu vipi Kwake kukupea Roho Mtakatifu kwanza."

147 Huenda ukaiga Roho Mtakatifu na ukatende kama mtu aliye na Roho Mtakatifu, lakini kama una Roho Mtakatifu, Mungu ajua mwanzo wako tangu mwisho. Hiyo ni kweli! Hiyo ni njia mbovu ya kuendesha shughuli. Mungu haendeshi Yake hivyo . . . Yeye alijua mwisho tangu mwanzo na alijua kila kitu kitakachowahi kuwepo hapa. Kila ua, kila mbu atakayewahi kuwa duniani, Yeye alijua hayo kabla ulimwengu haujaanza. Kwa hivyo mnaona, Yeye angeendeshaje shughuli zake hivyo. Yeye hafanyi hivyo.

148 Ukichunguza—kama kweli una Roho Mtakatifu, umeokolewa milele. Naweza kuthibitisha hilo Maandikoni mwote, na tumefanya hivyo mara nyingi. Lakini kusudi kuhifadhi wakati tukafikie maswali haya, huenda nikasema hili (mwaona?), kuwa mtu huyu alisema, "Vema, basi ungesemaje kuhusu Sauli?"

149 Nikasema, "Hakika Sauli alikuwa ameokoka." Nikasema, "Kumbuka, Sauli alianguka; nitakubali hilo. Yeye alianguka na akaenda mbali na Mungu, kwa sababu yeye alikuwa mwenye tamaa sana, Yeye alipenda pesa." Yeye alileta hizo dhabihu zote na kadhalika, wakati Samweli kwa Neno la Mungu alimwambia aangamize kila kitu. Lakini yeye hata alimwacha mfalme na akahifadhi vitu vingi na akivileta kwa sababu . . . Ona? Badala ya kufuata vile Neno la Mungu lisemavyo hasa, unaweka maoni yako ndani yake; hapo ndipo unapoanguka.

150 Hilo ndilo ninalowaza kuhusu madhehebu na kadhalika, wao walianguka, kwa sababu hawalifuati Neno. Na ukiwaonyesha Neno, wao wanalipa kisogo, kasema, "Ee, kanisa letu hufundisha *hivi*." Hilo si sahihi, ni yale Mungu alisema!

151 Basi Samweli aliagizwa kwenda kule—au Sauli alikuwa—na kuangamiza kila kitu kabisa, "Kila kitu, muangamize vyote." Badala ya kufanya hivyo, yeye akahifadhi baada ya dhabihu, kisha akasalimisha maisha ya mfalme, naye akafanya kila kitu. Basi Samweli alimwendea na kumwambia Roho wa Mungu alikuwa amemwondokea na—na mambo kama hayo.

152 Hatimaye Samweli akafa. Basi yapata miaka miwili baadaye, vema basi, Sauli alikuwa . . . Roho wa Mungu alimwondoka, bali yeye hakupotea. Hakika, yeye hakupotea, ule upako ulimwondokea. Sasa tazama, na uone kama ilikuwa hivyo sasa.

153 Sauli alienda mbali sana na Mungu hata alipoenda vitani . . . Yeye akajiandaa kwenda vitani. Naye alikuwa na wasiwasi kuhusu kuenda vitani, naye a—akamwomba Bwana ampe ndoto. Bwana hangempa ndoto. Hapakuwepo manabii nchini siku hizo, hamna nabii. Samweli alikuwa nabii. Wao walikuwa na watoa unabii, bali—na lakini wao—yeye hangepata jibu toka kwa Mungu kwa njia yo yote. Hata alienda kwa Urimu Thumimu na kuuliza pale. Wala kule kumetameta kwa umeme juu ya Urimu Thumimu hata hakungemjibu. Basi yeye alifanyaje? Alienda kifichifichi hata pangoni mwa yule mchawi, mpiga ramli. Naye huyu mchawi . . . Yeye alijigeuza kuwa mtumishi na akaenda kule, kisha akasema, "Tafadhali nipandishie roho ya nabii Samweli?"

Naye mwanamke yule akasema—akasema, "Vema sasa, wajua aliyosema Sauli." (Yeye alikuwa akiongea na Sauli, lakini hakumjua.) "Sauli alisema wote walio na roho wa upambanuzi, hawana budi kuuawa."

Alisema, "Nitakulinda toka kwa Sauli, lakini nipandishie roho wa Samweli."

Kwa hivyo yule mchawi akanza kufanya uchawi wake, na muda si muda, yeye alipomwona Samweli akitokea, roho yake ikija, ikionekana wazi mbele yao, yule mwanamke alisema, "Naona miungu inatoka katika nchi."

154 Hiyo ni mojawapo wa faraja. Mtazame mzee Samweli amesimama pale. Yeye alikuwa tayari amekufa kwa miaka miwili, lakini yeye alisimama pale. Si tu... Yeye alikuwa amesimama pale amevalia vazi lake la unabii. Sio tu ya kwamba yeye alikuwa hai, bali alikuwa yuangali nabii. Haleluya!

Yeye alisema, "Umenidanganya." Kasema "Yule..."

Basi Sauli alisema, "Samweli, sijui la kufanya; naenda vitani kesho, naye Roho ameniacha." Akasema, "Siwezi hata kupata ndoto toka kwa Bwana. Na ile Urimu Thumimu haitanizungumzia mimi. Mimi niko katika hali mbaya mno."

155 Yeye akasema, "Kwa kuwa umekuwa adui wa Mungu, kasema, mbona umeniita toka mapumzikoni mwangu?" Ona? Samweli alisema hayo. Kasema, "Mbona uliniita toka mapumzikoni mwangu, nawe umekuwa adui wa Mungu?" Ndiposa akashika kumwambia. Akasema... Lakini hata hivyo, yeye angemwambia Sauli Neno la Bwana. Naye alipofanya hivyo... Sasa kumbuka, yeye alikuwa tayari amekufa miaka miwili. Ona? Lakini yeye alisema, "Nitanena Neno." Yeye akamwambia Neno la Bwana. Kasema, "Kesho utaangamia vitani, na Yonathani mwanao ataangamia pamoja nawe." Na, yeye akasema, "Kesho usiku wakati kama huu utakuwa pamoja nami." Kama yeye alipotea, hata na nabii Samweli pia. Hilo ni la kiasili; mwaona sababu inaitwa hivyo. Ona, Ona? Yeye alisema, "Utakuwa pamoja nami kesho usiku wakati kama huu." Ona? Basi kama Sauli alipotea, hata na Samweli pia, kwa sababu wao wawili walikuwa mahali pamoja.

156 La, la! Watu wa Kiasili, ninyi... Mnaojiita wa Kiasili, kama wanavyojiita Church of Christ, na wanaojiita Wakristo, unaodhaniwa kuwa Ukristo. Siku hizi kwa sababu u Mwamerika unadhaniwa kuwa Mkristo, kwa sababu wewe—wewe ni Mwamerika. Ona? Huo—huo ndio unaoitwa Ukristo. Lakini Mkristo halisi ni mwanamume aliyezaliwa mara ya pili kwa Roho na mwanamke aliyezaliwa kwa Roho. Hilo hasa... Hawa wengine wanaiga, lakini Wakristo halisi huitwa na Mungu.

**157. Tafadhali eleza tofauti kati ya roho na nafsi.**

157 Vema sasa, hilo ni gumu. Lakini kwanza wewe ni kiumbe cha utatu, kama tu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni vyeo vitatu vinavyohusu mtu mmoja, ambaye ni Yesu Kristo. Nawe u nafsi, mwili, na roho. Lakini inachukua hivyo vitatu kukufanya wewe. Na ukiwa na kimoja cha hivyo tu, wewe si wewe. Inahitajika vyote vitatu kukufanya wewe.

158 Kama nilivyosema hivi majuzi, "Huu ni mkono wangu; haki ni kidole changu; hili ni pua langu; haya ni macho yangu; lakini *mimi* ni nani?" Mimi ni nani ambaye hivi ni vyake? Ni kile kilicho ndani yangu; hiyo ni ile—ile busara.

Kama jicho hili, kama mikono hii, kama mwili huu ungesimama hapa kama tu ilivyo leo, hata hivyo ni—ninge-. . . Mwili wangu ungekuwa hapa, lakini *mimi* ningekuwa nimeondoka, mimi nilivyo. Vile—ye yote niliye ndani yangu ameondoka. Hiyo—hiyo ndiyo sehemu—sehemu ambayo ni roho. Nafsi ni tabia ya huyo roho, ndipo Roho Mtakatifu anapokujilia, haifanyi lo lote . . . Wewe . . . Anakubadili au anageuza roho yako kuwa nafsi tofauti. Na hivyo nafsi ni tabia tofauti iliyo kwenye hiyo roho. Kwa hivyo nafsi ni tabia ya roho yako.

159 Kwanza ulikuwa mchoyo, mwovu, na mwenye chuki, na hila, na ubishi; sasa wewe u mwenye upendo, mzuri, mkarimu, na—na . . . Mwaona tofauti? Ni tabia yako. Tunge-. . . Nitaiita hivyo. Ni nafsi yako iliyogeuzwa. Ile nafsi ya kale ilikufa, na nafsi mpya ambayo ni tabia mpya ikazaliwa ndani yako. Ona?

160 Ubongo wako sio busara yako; roho yako iliyo ndani yako ndiyo busara yako. Ona? Ubongo wako ni tita la vitu vya kinyama na chembechembe na vinginevyo; hauna busara wenyewe. Kama ungekuwa nayo, basi mradi tu umo mle, au umekufa au u hai, bado ungefanya kazi. Ona? Lakini si—si ubongo wako; ni roho yako ndani yako. Na nafsi yako ndiyo tabia ya huyo roho. Hiyo ni nafsi ya roho inayoongoza—ile roho inayoungoza mwili. Ona? Naam.

Sasa, yanipasa niharakishe, kwa sababu tunachelewa kidogo. Sasa, nadhani kuwa—natumai hilo litashughulikia hayo.

**158. Ndugu Branham, tafadhali fafanua—tafadhali eleza kama wanawake wanapaswa kushuhudia au kunena kwa lugha katika kusanyiko.**

161 Vema, naamini kuwa kama mwanamke huyo ni m—mhubiri katika hilo kusanyiko, yeye hapaswi kuwa mhubiri. Lakini kama yeye ana karama ya lugha na anena katika makutano, ambapo kuna—kuna manabii na—na karama zimekusanyika pamoja, naamini yeye ana haki kufanya hivyo. Kwa sababu katika Biblia twaona kuwa walikuwa na manabii wa kike kama Miriamu na wengineo, nao hawakuwa—hawakuwa na mamlaka . . . Nikifikia mahubiri yangu madogo hapa, ni—nitaingiza hayo ndani mle. Ona?

162 Lakini wanawake, kama wana karama . . . Sasa, njia sahihi ambayo naamini kuwa tutakapokusanyika hivi punde . . . Kanisa letu litakapoimarika kidogo zaidi . . . Na—na hata hivyo, kuna kikundi kipya—kanisa lingine huenda litajiunga na . . .?. . . kujiunga na kanisa hili mara tu tupatapo nafasi hapa kwao na kadhalika. Kanisa lingine litakuja liungane na kanisa hili, si dhehebu, linakuja tu kama mwili, katika kundi, kanisani. Na—na ni kundi la watu walio na karama.

163 Na sasa, litakapoungana pamoja, jambo la kufanya, ni kwamba hawa watu walio na karama yapasa wakutanike nyakati fulani wao wenyewe, waone roho atawaambia wao nini.

Ndiposa itaelezwa toka jukwaani. Na watu wale. . .Ni kwa ajili ya kulijenga kanisa.

164 Sasa, ukinena kwa lugha, na unajua, hakuna ye yote wa kuzifasiri. . .Ndiposa unapokuwa katika mikutano, wakati mwingine hamna unyenyekevu, mwajua. Unaona wakati mwingine. . .Nimekuwa nikisimama katika kusanyiko langu kutoa wito wa madhabahuni, na mtu fulani angesimama na kuharibu huo wito wa madhabahuni kwa kunena katika lugha. Sasa ona, sasa mtu yule huenda amekuwa akinena kwa lugha sahihi; huyo huenda alikuwa Roho Mtakatifu, lakini mwaona, bila kufundishwa kujua la kufanya, jinsi ya kushikilia hilo. . .

165 Nimeketi jukwaani na kusikia mhubiri akihubiri na kumwona yeye akifikia mahali. . .Lo, nilitaka kusimama na kumsaidia sana hata sikujua la kufanya. Na mmefanya jambo lile lile; sisi wote hufanya hivyo. Lakini ni nini? Huko ni kukosa unyenyekevu. Keti chini. Mheshimu ndugu yangu.

166 Nilisikia—nilimsikia Ndugu Neville akihubiri, naye amenisikia nikihubiri wakati ambapo, si shaka, tunge-. . . Ndugu J.T. hapo na wengineo, au—hao wote, twaweza kusikia sisi kwa sisi tukihubiri, tuwazie, "Ee, ndugu, naamini nitasimama nikamsaidie." Ona? Unasikia tu Roho akimiminika juu yako, lakini unafanyaje? Tulia. Ona? Kwa sababu roho wa manabii huwatii manabii. Ona? Hiyo ni kweli, nyamaza. Ona? Fanya hivyo.

167 Lakini naamini kama mwanamke. . .Swali lilikuwa kama mwanamke yule ana kipawa cha lugha na anataka kunena, naamini kuwa wakati huo ufikapo, yeye ana haki ya kunena katika kipawa cha lugha, lakini si kuhubiri au kumtawala mwanamume. Anapokuwa mhubiri, bila shaka anamtawala mwanamume.

**159. Ndugu Branham, nilimwoa mwanamke aliyekuwa ameshaolewa hapo awali. Tuliachana, naye ameshaolewa mara mbili tangu wakati huo. Biblia inasema tukitaka kuoa—tukitaka kuoa, kurudia yule. . .mke wa kwanza. Sasa, naweza kumrudia yeye ambaye ameolewa hapo awali au naweza kuwa huru?**

168 Vema, sasa, ndugu yangu, hapa kuna njia pekee ambayo ungefanya. Sasa, hili ni somo kuu, na siku moja ni—ninataka ku—kanisa litakapokuwa katika taratibu na limetengenezeka hata kufikia mahali panapofaa au. . .Ni—ninasema hili kwa unyenyekevu, ni. . .Kuna makundi mawili ya ndoa na talaka makanisani, moja lashikilia upande mmoja na lingine mwingine. Basi nionavyo mimi, kwa neema, iliyo moyoni mwangu mbele za Mungu na Biblia Yake, yote mawili yamekosea. Ona? Lakini kuna kweli iliyopo pale.

169 Ukichunguza yale Yesu alisema. . .Sasa hapa, nina ndugu, ndugu yangu kwa kuzaliwa, anayejiandaa kumwoa mwanamke.

Na ndugu yangu alikuwa ameoa hapo awali na ana mtoto kwa mwanamke mzuri. Naye alinijia niwaoze. Nikasema, “La, haiwezekani kabisa!”

170 Yesu alisema katika Mathayo 5, “Kila mtu amwachaye mkewe, na kumwoa mwingine, isipokuwa kwa habari ya uasherati (ambao yeye alifanya kabla yeye hajaolewa na hakumwambia mtu huyo), amfanya kuwa mzinzi; na mtu akimwoa yule aliyeachwa, azini.” Kwa hivyo msifanye hivyo. La, huwezi kurudia mke wako wa kwanza kama yeye amekwisha olewa tena. Lakini uki—kama yeye alikutaliki na kukuacha . . .

171 Ndipo ulisema, “Mimi ni huru?” Hebu nilisome tena. “Nilimwoa mwanamke ambaye alikuwa ameshaolewa hapo awali. Tuliachana, naye ameshaolewa mara mbili (nadhani mtu huyu amebaki tu mseja). Biblia inasema kuwa tukitaka kuoa tumrudie yu . . . yule wa kwanza.”

172 La, bwana! Tazama torati za Walawi. Ukimrudia mwanamke huyo yeye ni mali ya mtu mwingine. Umejichafua na kujifanya mbaya zaidi ya ulivyopata kuwa. La, haupaswi kumchukua mke ambaye ameshaolewa na mtu mwingine.

173 Sasa, “Je, nimrudie yeye ambaye ameshaolewa hapo awali au niwe—au niwe huru?” U huru! Kaa huru! Naam, usimrudie tena. La, bwana! Yeye ameshaolewa na mtu mwingine; usimkaribie. Naam! Usi- . . . Hilo linachafua . . .? . . . Mwafahamu. Kama tungalikuwa na wakati zaidi kidogo, ningetaka kuingilia hilo. Lakini kwa swali lako, ndugu yangu, ye yote yule. La, bwana! Usimrudie na kumtwaa mwanamke huyo hali ameshaolewa mara mbili au tatu tangu ulipomuoa. Hilo ni kosa.

174 Niliwaoza mume na mke hapa si muda mrefu uliopita ambao walikuwa wameoana hapo awali, nao walitalikiana na kuachana, na—mume na mke wazee. Ee, ilikuwa Ndugu na Dada Puckett; ndio hawa hapa hasa. Hawangesikizana na walikuwa na mzozo mdogo kati yao; wakatalikiana. Mwanamke yule aliishi kiaminifu akiwa pekee kama alivyoweza, na mumewe aliishi vivyo hivyo. Hatimaye, waliona jinsi walivyokuwa wapumbavu, nao wakarudi na kutaka kuona. Nilisema, “Hakika!” Ona? “Naam, hivyo ndivyo wapaswa kuwa.” Kwa hivyo wao . . . Vema, walikuwa wameoana wakati wote. Hawakuwa wametalikiana kamwe; niliwapa tu makaratasi waishi pamoja kama mume na mke; hivyo tu, kwa sababu walikuwa wameoana mwanzoni.

**160. Zile herufi tatu kwenye msalaba wa Katoliki zina maana gani?** (Hebu tuone.) **Zile herufi tatu kwenye msalaba wa Katoliki zina maana gani?**

175 Vema, nadhani misalaba yote ni sawa, kama sija- . . . Yapasa nichunguze hayo. Lakini una I-R-N-I ambayo maana yake ni “Yesu wa Nazareti, Mfalme wa Wayahudi.” Ona? Kama hivyo ndivyo ilivyo, sikujua kulikuwa na zingine maarufu, wala cho chote kile. Lakini hizo herufi maana yake ni “Yesu wa

Nazareti, Mfalme wa Wayahudi." I-R-N-I, hizo ndizo zilizo kwenye msalaba. Vema.

**161. Ni kosa kutumia fungu la kumi kwa hazina ya ujenzi wa kanisa?**

176 Vema, sasa, hapa—hapa kuna kitu kidogo cha tahadhari kwa kanisa sasa. La, fungu la kumi linapaswa kumwendea mhudumu. Hiyo ni kweli! Katika Biblia walikuwa na kijisanduku walichokuwa wa mekiweka mlangoni katika Agano la kale wakati wa—wa ujezi. Sanduku hili lilikuwa hazina ambamo watu waliweka mle kwa ajili ya kutengeneza... Mmesoma hayo mara nyingi katika Agano la Kale. Walitunza manyumba na kadhalika hivyo...Kurekebisha majengo kwote kulishughulikiwa kwa hazina hiyo. Lakini fungu la kumi ya hizo ilienda—sehemu ya kumi ya hilo fungu la kumi—zaka zote zilienda kwa makuhani, wachungaji wao. Naam, fungu la kumi halipaswi kuenda kwa jambo lingine lo lote.

177 Najua watu hulichukua fungu lao la kumi na kuwapa wanawake wajane. Hilo ni kosa. Kama una cho chote cha kumpa mwanamke mjane, mpe, ila usimpe pesa za Mungu. Hizo kwanza si zako. Hizo ni za Mungu!

178 Ukinituma mimi kule mjini kununua mkate, na unipe senti ishirini na tano kununulia mkate, nami nikutane na mtu fulani barabarani anayeuhitaji...kitu kingine, na kama ningempa zile senti ishirini na tano, ona, ningewapa pesa zako. Kama waliniomba kitu, basi na wakipate toka kwa mfuko huu na niwape pesa zangu; lakini hizi ni pesa zako. Na sehemu yake ya kumi ni ya Bwana. Naye Lawi, yule kuhani, angeishi kwa ile sehemu ya kumi.

179 Ile sehemu ya kumi yapaswa kuwa zaka ambayo italetwa ghalani pamoja na ahadi ya Mungu ya kuibariki, na kujaribia. Yeye alisema, "Kama hauniamini, njoo unijaribu uone kama sitalifanya." Ona? Hiyo ni kweli.

180 Fungu la kumi huenda kanisani kwa ajili ya mchungaji na kadhalika kuishi kwayo. Ndiposa ha—ha—hazina ya mijengo na kadhalika ni hazina tafauti kabisa. Sasa, hilo—hilo ni kulingana na Maandiko.

181 Wakati mmoja tukiwa tayari nataka kuchukua usiku... Nilienda hapa wakati mchache uliopita kabla sijaachana na maskani haya na kuchukua karibu majuma mawili au matatu kwa somo kama hilo na kulieleza lote na kuonyesha fungu la kumi ni nini kanisani.

**162. Ndugu Branham kuna ubaya wo wote kuwa mshiriki wa chama fulani baada ya kuwa Mkristo, kama kile cha Masons?**

182 La, bwana! Uwe Mkristo ko kote uliko. Sijali uko wapi, unaweza kudumu ukiwa Mkristo.

**163. Unafikiri njia nzuri ya kumpata Bwana ni ipi . . . Waonaje—unafikiria ni ipi njia bora zaidi ya kutafuta mapenzi ya Bwana katika mambo muhimu**

Sasa, hebu . . . Siamini ninge . . . Hebu nione kama naweza kupata mwendeleo wake, "Unafikiri ni ipi njia nzuri (naona kungekuwa na alama ya kupumzika pale, nadhani) . . . Unafikiria ni ipi njia bora zaidi ya kutafuta mapenzi ya Bwana katika mambo muhimu?"

183 Nakwambia, rafiki mpendwa, njia bora zaidi ya kutafuta mapenzi ya Mungu katika mambo muhimu ni kuomba. Ona?

184 Sasa, hebu ni- . . . Hapa kuna jambo ndogo la ajabu hapa. Kama una—kama—kama una jambo ambalo ni muhimu sana . . . Sasa, utafanya hivi. Mimi hulipeleka mbele za Bwana. Na kila mara imekuwa nguvu zangu; namngoja Bwana na kuona atasemaje. Nami simo, sichukii upande wo wote, na kusema, "Sasa, Baba wa mbinguni, ya—yaweza . . . "

185 Hakika sasa, katika hali yangu wakati mwingi, kama ni muhimu sana, nangoja ono. Lakini watu wengi, Mungu hawashughulikii kwa maono. Kwa hivyo basi, singewashauri ninyi kufanya hivyo. Ona? Kwa sababu ni watu wachache tu walio na maono na wengine hufanya jambo lingine. Ambapo unafanya kitu kingine ambacho singalifanya, labda—katika njia yako ya kumtumikia Bwana—Mimi hufanya jambo lingine ambalo hungelifanya. Ona? Mungu hutushughulikia kwa njia mbalimbali.

186 Na kwa hivyo kama ningelikuwa mahali pako na sikuwa na maono toka kwa Bwana, ningemngoja tu Bwana na kusema, "Bwana, sasa unionyeshe nitafanya uamuzi gani." Ndiposa, jinsi unavyojisikia ukiongozwa kufanya, ndipo ngoja kidogo, ndiposa ngoja zaidi, na uone ni njia ipi, unaegemea upande upi, upande upi Roho . . . Useme, "Sasa, Baba, moyoni mwangu wewe wajua haijalishi; lakini ni—ninataka kujua kile Wewe unataka kufanya kuhusu hilo."

187 Hivyo ndivyo ninavyofanya kuhusu mikutano wakati mwingine. Kama ninajisikia nikiongozwa kuenda hivi au hivyo, basi nitafuata hiyo. Hivyo ndivyo ipaswavyo kuwa, kwa sababu ni katika maombi basi; unafanya vizuri sana uwezavyo.

188 Nimi naamini hili rafiki zangu, kama Paulo alivyokuwa katika—katika Agano Jipya katika siku zilizopita. Yeye alikuwa amekwama, hajui aende wapi. Naye akaanza kufuata njia mbaya, naye akapata wito wa Makedonia. Nami naamini kama unafanya uamuzi kwa Mungu na ufanye uwezavyo, naamini Mungu atakusahihisha na usi-—aone kuwa hukosei. Naamini Mungu atafanya hivyo.

**164. Hebu tuone. Ndugu Branham, itakuwaje kwa watu ambao—watakaohesabiwa kuwa wanawali waliolala wakati watakapohukumiwa kwenye ile hukumu?**

189 Vema, wale wanawali waliolala wataokolewa bila shaka. Wataokolewa hukumuni. Hawatakuwa Bibi-arusi kamwe, lakini hao ni kundi la watu liliookolewa ambalo litakuja hukumuni, ambalo halitahesabiwa katika Bili arusi. Bali mradi tuo hao ni bikira, wako mbele za Mungu. Ona? Wataokolewa. Watabaguliwa. . . Watakuwa ndio wale kondoo walio kwenye mkono Wake wa kuume. Na wale wasiookoka watakuwa mbuzi kwenye mkono wake wa kushoto kwenye ile Hukumu ya kile Kiti Cheupe cha Enzi.

Ningechukua wakati mwingi kwa hayo, bali mimi—kunachelewa sana.

**165. Inawezekana kwa mtu aliyejazwa Roho Mtakatifu kupeperushwa na—kupeperushwa na—kufanya vitu vidogo. . . kushawishiwa kufanya mambo madogo—mambo madogo ambayo yeye hataki kufanya?**

190 Ee, naam! Naam, bwana! Ndivyo, mtu aliyejazwa Roho Mtakatifu. . . Unaweza kuwa—kupeperushwa na vitu hivi. Unajifanya shabaha. Unapokuwa chini pale ukitumikia ibilisi, yeye anakuacha tu uhangaike hapa na pale vyo vyote utakavyo, lakini wakati mmoja ulichukua msimamo kwa ajili ya Kristo. Umeenda upande mwingine basi; Yeye amekuelekezea na kukuzungushia kila bunduki. Kila jaribu, kila kitu ambacho ungetupiwa, unakipata. Lakini una nini? "Yeye aliye ndani yako ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia." Ona?

191 Sasa, haukuwa vitani hapa, ulikuwa tu ukigaagaa ovyo. Ona? Lakini sasa, ume—umeoshwa, umejipamba; umenyolewa; umechana nywele yako; umevaa vazi rasmi; una bunduki mkononi mwako. "Haya twende!" Ona. Uko vitani, si kujionyesha, lakini kupigana, basi pigana! Hakika majaribu yatokeapo, pamoja na roho—ngao ya imani, bizimu. . .?. . . na usonge mbele." Ona? Naam. Ee, jitwike silaha zote za Mungu. Mbona uchukue silaha kama huendi vitani? Wanajeshi wote hujivika wapigane, si kujionyesha, kuenda nje na kusema, "Mimi ni *fulani wa fulani*. Sasa, Mimi ni Mkristo. Ona nilivyo. Mimi ni wa *hiki,* na *kile*. Haleluya! Nilimpokea Roho Mtakatifu usiku uliopita. Hakika, hakuna lo lote linaloniudhi tena." Enhee! Ee, ndugu, na—naamini unapaswa kurudi nyuma ukajaribu tena. Ona?

192 Ee, nakwambia, mara tu unaposema una Roho Mtakatifu; Shetani anakuelekezea kila bunduki, akikupiga risasi. Ndipo uwe umejivika silaha zote, ndipo chukua ngao ya imani, upanga wa Roho au Neno, na jivike bi—birizi kwa—umejivika Injili, na uweke kile kipande kingine cha katikati cha kale hapa, dirii, na jihakikishie hayo, kisha ujikaze kidogo, na ujiweke tayari kwa sababu yanakuja. Usiwe na wasiwasi. Naam, bwana! Utapata shinda nyingi sana. Lakini kumbuka, "Yeye aliye ndani yako ni mkuu, kuliko yeye aliye katika dunia."

**166. Yesu alimaanisha nini katika Ijili ya Mathayo 16:9 na 10? Vile vikapu kumi na viwili na vile vikapu saba vinawakilisha nini? Swali la Jumapili asubuhi.**

193 Hebu tuone—hebu tuone, Mathayo 16:10. Sina hakika sana hivi sasa. Hebu tupate yalipo, Mathayo 16:9 na 10-16:9 na 10. Ndiyo hii.

> *Hamjafahamu . . . bado, wala hamkumbuki ile mikate mitano kwa wale elfu tano, na vikapu vingapi mlivyoviokota?*
>
> *Wala ile mikate saba kwa elfu nne, na makanda mangapi mliyoyaokota?*
>
> (Sasa tazama. Hebu tuchukue mengine kidogo kabla haya.)
>
> *Yesu akawaambia, Angalieni, jilindeni chachu ya Mafarisayo na Masadukayo.*
>
> *Wakabishana wao kwa wao, wakisema. Ni kwa sababu hatukuchukua mikate.*
>
> *Naye Yesu* . . . (Sasa tazama!) . . .
>
> *Naye Yesu akafahamu,* . . . (Yeye alipata mawazo yao, mwaona?) . . . *akawaambia, mbona mnabishana ninyi kwa ninyi, enyi wa imani chache, kwa sababu hamna mikate?*
>
> *Hamjafahamu bado, wala hamkumbuki ile mikate kwa wale elfu tano, na vikapu vingine mlivyoviokota?*

194 Kwa maneno mengine ni hivi: "Kama mlimwona Mungu akitoa na kufanya muujiza, basi si Yeye aweza kufanya muujiza tena?" Ona? Ona, kama . . . kwa maneno mengine, hivi: "Kama Yeye alikuokoa wewe toka kwa maisha ya dhambi, je, Yeye hawezi kuuponya mwili wako? Haukumbuki ulipokuwa mwenye dhambi jinsi Yeye alivyoinua nafsi yako katika imani kuamini? Si Yeye vivyo hivyo aweza kukufanyia jambo kuu tena? Si Yeye aweza kukufanyia mu—muujiza au jambo lingine? Vile vikapu vitano . . ." Kasema, "Kumbuka . . ."

195 Kama . . . Walipovuka ile Bahari ya Shamu, Mungu alifungua njia hivyo na kufanya Bahari ya Shamu ifunguke hivyo, nao wakapitia humo, yeye alikuja ng'ambo ya pili, na mara tu alipokosa maji; walianza kunung'unika. Sivyo? Mara tu walipokosa chakula wakaanza kulia, "Hatuna chakula." Ona? Kasema, "Hamkumbuki miujiza ile nyuma kule kwenye Bahari ya Shamu? Hamkushuka . . ." Walipopata—walipofika mahali fulani karibu na Bahari ya Shamu, "Ee," wao walisema, "Hapana shaka tutakufa. Hapa waja Wamisri wakitukabili sisi sasa. Haya basi; tutafanyaje?"

196 Kasema, "Nani aliyepiga nchi kwa mapigo chini kule? Nani alilifanya jua liangaze kule Gosheni?" Ona? Yatupasa

kukumbuka mambo hayo kukumbuka Mungu ni Mungu! Haleluya! Hata iweje, Yeye yuangali Mungu. Yeye hakika aweza kufanya cho chote.

**167. Je waweza kufafanua ule "Mwili wa Kristo," katika I Wakorintho 12:27 na "Bibi-arusi wa Kristo" katika Ufunuo 2:9-9. Je, Yerusalemu mpya ni ya kiroho hapa katika—ni ya kiroho katika Ufunuo? Ni—ni—je, huku ni kupambanuliwa rohoni kwa Kanisa?**

197 La! Sasa, hebu tuone kama napata hili kwanza sasa, I Wakorintho upesi sana, I Wakorintho ile sura ya 12, vema, na kifungu cha 27.

> *Basi ninyi mmekuwa mwili wa Kristo, na viungo kila kimoja peke yake.*

198 Ndiposa, lilikuwa wapi Andiko lingine? Ufunuo 2-21:9, Ufunuo katika sura ya 21 na kifungu cha 9. Vema, ndiyo hii.

> *Akaja mmoja wa wale—akafa mmoja wa wale malaika saba waliokuwa na vile vitasa vilivyojaa yale mapigo saba ya mwisho, naye akanena nami, akisema, njoo huku, nami ni—ni—nitakuonyesha yule Bibi-arusi, mke wa Mwana-Kondoo.*

199 Naam, ule Mwili wa Kristo. Ona, ule mwili wa Kristo uliovunjwa kwa ajili ya dhambi zetu na kwa Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa Mwili huo na kufanyika washiriki. Na mwili huo uli—uli—huo mwili . . . Mke wangu, tukinena kwa mfano . . . Hawa alitoka wapi? Mwili wa Adamu. Yeye alitolewa ubavuni mwake. Yule Kristo . . . Naye alikuwa sehemu ya mwili wake. Yeye alisema, "Yeye ni mwili wa mwili wangu na mfupa wa mifupa yangu. Nami nitamwita mwanamke." Ona?

200 Sasa, na Mwili wa Kristo ulitolewa kwenye mwili wa Yesu, maana sisi tu roho na mwili na mifupa Yake. Ona? Kwa sababu sisi tumezaliwa kuwa Mwili Wake. Na kwa sababu mwili huu hapa ni Wake, ingawa umezaliwa katika dhambi, Yeye ameukomboa. "Mungu ataufufua katika siku za mwisho nami nitaishi ndani yake milele." Ona? Naam. Vema.

201 Sasa, hebu tuone, swali la mwisho hapa lilikuwa: "Je, Yerusalemu mpya ni ya rohoni?" La, la, Yerusalemu mpya, Yohana aliiona ikishuka toka kwa Mungu Mbinguni; sikupambanuliwa kwa kanisa sasa. Mwaona? Ni—ni—ile . . . Ile Yerusalemu aliyoiona Yohana ikishuka toka Mbinguni imetayarishwa kama—Ufunuo 21 (ona?)—imetayarishwa kama Bibi-arusi aliyekwisha kupambwa kwa mumewe . . .

Swali la mwisho sasa; nadhani yamekwisha.

**168. Biblia husema kuwa cho chote kinachotendeka huwa kwa manufaa ya wale wampendao Bwana. Basi kama unampenda Mungu na ukarudia ulimwengu je, Mungu**

**atakuacha ufie dhambini au Yeye atakurudisha Kwake kabla hajakutwaa?**

202 Bibi huyu aliandika jina lake, kwa hivyo ningesema mwa—mwanamke fulani (ona?), kwa sababu yeye aliandika jina lake. Naam, Dada. Kama umezaliwa . . . Sasa, hebu nipate hili. Ona, kwa kitambo kidogo, muda mdogo, kila mmoja wetu huanguka mara nyingi kwa siku. Twajua hilo. Sisi sote tuna hatia, kila mmoja wetu; hakuna mmoja wetu aliye mkamilifu. Na mradi tu tuko katika mwili huu, sisi tungali . . . Hata watu wajaribu kusema vipi, "Nimetakaswa; naweza kumbusu mwanamke huyo au nifanye hiki." Yeye anadanganya; hawezi. Naam, hivyo tu.

203 Sijaribu kusema, "Bwana, hebu nione naweza kukaribia vipi." Ni, "Bwana niweke mbali sana niwezavyo kuwa." Ona? Hebu tu kaa mbali sana kama . . . kumbuka, wewe bado u mwanadamu. Ona?

204 Na . . . Lakini sasa, ukikosea na kufanya kitu kibaya . . . Hufanyi kwa kupenda . . . Kama u Mkristo, kama wewe ni Mkristo aliyezaliwa mara ya pili, hukusudii kufanya kosa. Nia yako na kila kitu ni sawa. Lakini ukifanya hivyo, kama mwanamke huyu alivyosema hapa, ukifanya kosa na utende jambo fulani baya, je, Mungu atakuacha uendelee na ufe hivyo ukapotee, au Yeye atakurudisha tena kwa kukupatanisha? Yeye atakurudisha. Naam! Yeye atakurudisha.

205 Na kama—ndiposa, ukifanya cho chote kibaya, hakikuhukumu na unaendelea hivyo, nje kule, kumbuka, haukuwa umeokoka tangu mwanzo. Naam. Hu—hukuwa—hukuwa umeokoka; ulijifanya tu; haukuwa umeokoka. Lakini unapookoka, una roho tofauti; una tabia tofauti. Wewe u kiumbe kipya katika Kristo, na ya kale yamepita, nayo yamekufa na kuzikwa katika ile bahari ya usahaulifu. Mwaona?

206 Wala . . . Lakini kwa kuwa unaishi humu ulimwenguni, kuna mitego uliyowekewa kila mahali, nawe unatembea hali macho yako yameelekezewa Kristo. Basi kumbuka, unapofanya kosa, Mkristo halisi kila mara atarudi upesi kwenye upatanisho.

207 Tazama, katika safina ile Mungu alimwachilia kunguru wa kale kuondoka—au Nuhu alimwachilia kunguru aende. Sasa, yeye alikuwa nani? Yeye alikuwa kunguru. Ee, naam, yeye alilala kwenye kiota kile kile pale pamoja na yule hua. Wote wawili walikaa katika kiota kimoja; lakini alipomwachilia yule kunguru wa kale aondoke, vema, mzee . . . Nawazia maji yote yalikuwa na uvundo wa mamilioni ya watu iliyovimba na kuoza juu ya maji, na farasi na wanyama wote wafu. Ulimwengu wote uliangamizwa. Basi ndiyo hapo, hii mizoga ya kale ikielea juu ya maji na vitu kama hivyo. Kisha Nuhu akamwachilia hua, kwa sababu yeye alidhani aliona nuru ya jua. Naye alitaka kujua kama maji yalikuwa yamepungua au la, kwa hivyo yeye alimwachilia yule—yule—yule kunguru. Naye maskini kunguru

alipurukia mzoga mfu wa kale, "Lo, vema tu; hilo ni zuri!" Ona, kula mzoga. Mbona? Hiyo ilikuwa tabia yake. Yeye alikuwa kunguru. Haijalishi angekaa pamoja na hua muda gani, ni mara ngapi alisikia Nuhu akihubiri, ni muda gani angeketi na ndege wasafi, yeye alikuwa kunguru tangu mwanzo. Mara tu yeye alipopata nafasi kuonyesha hali yake, yeye akaionyesha.

208 Naam, lakini yeye alipomwachilia yule hua, alipoanza kutoka tu, wee, yeye hangeistahimili. Hakuwa na pa kwenda; hangepata pa kutuliza nyayo za miguu yake, kwa hivyo akarudi safinani. Na hivyo ndivyo iliyo.

209 Wakati mwingine huenda ukaachiliwa kidogo kuona kile ungefanya, lakini wewe kila mara kama una tabia ya hua, huwezi kula chakula cha kunguru. Naam, hakitatulia tumboni; hivyo tu.

210 Ungeenda wapi, ungetenda nini? Niambieni kile ungefanya kama ungekuwa—kama haungelikuwa Mkristo! Niambie yale ningefanya asubuhi hii kama sikuwa Mkristo! Ningefanyaje asubuhi ya leo na mama yangu amelazwa kule hospitalini katika hali hiyo na amepotewa na fahamu hivyo na amelala pale, na moyoni mwangu ningesimama hapa mimbarani na kuhubiri na kuendelea jinsi nifanyavyo, inaonekana kama sijali hayo sana? Kwa sababu ninajua mama yangu ameokoka. Ona? Ninajua Yeye ameokoka. Namjua Yeye ninayemwamini; ninasadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana Kwake hata siku ile.

211 Mama angefanyaje sasa? Sasa, labda huenda alikuwa na nia nzuri maishani mwake mwote, ya kwamba "Siku moja nitakuwa Mkristo." Lakini angekuwaje sasa anapolala pale huku amepotewa na fahamu? Angekuwaje Mkristo sasa? Watoto wake wangefanyaje?

212 Majuzi tulipomweka—tulipompeleka nje kule kumpa maji ya sukari nje pale. . .Hicho ndicho kitu pekee ambacho kimo mwilini mwake ni ile sukari. Hawezi kumeza; amepooza. Naye alisema, "Nakutaka ujue jambo hili moja, Billy." Yeye alinena kunihusu mimi huku Delores amesimama pale, na juu ya watoto wake na mengineyo, na juu ya watoto wake na mengineyo, na baadhi ya ndugu zangu wanaokunywa pombe.

Nilisema, "Vema, wameuvunja moyo wake."

Yeye alisema—akasema, "Lakini Billy, hayo yote huingia katika gurudumu la mama." Kasema, "Lakini nimeokoka." Kisha akasema, "Niko tayari kwenda."

213 Nilisema "Mama, huenda ungelituachia nyumba yenye ukubwa wa kutoka Jeffersonville hata Utica, jumba la enzi; huenda ungelituachia dolla milioni kuzozania na kung'ang'ania ukisha ondoka (hayo tu ndiyo yangetendeka kwa hizo); lakini Mama, umetuachia hazina kuu zaidi ambayo mtu ye yote angeacha, ma—matumaini kwamba tutakuona tena katika nchi ile ng'ambo ya mto." Hiyo ni kweli! Ona?

214 Umeokoka, na nina furaha sana kujua kuwa Kristo huokoa. . . Lakini huenda tukaanguka; huenda tukafanya makosa; sisi sote tuna heri na shari zetu; lakini nafsini mwako mara tu ufanyapo kitu fulani, vema, kuna kitu fulani kinachoharibika ndani yako; wajua ndivyo ilivyo. Sasa, hapo ni wakati wa kuruka. Huo ndio wakati wa kuruka. Kiondokee.

215 Sasa, tuseme unaenda nje hapa leo, na—na mtu fulani aje na kusema, "Hee, usiniambie wewe u mmoja wa watakatifu wanaojigaragaza."

Mara, Shetani anasema, "Mchape kofi!" Ona?

216 "Sijui kuhusu mtakatifu anayejigaragaza; Mimi ni Mkristo!" Ona? Na kila mara kwa uovu, ukabili uovu kwa wema. Na kumbuka, sasa chukua tu hili, unapoukabili uovu kwa wema, uovu hauwezi kusimama mbele ya wema. Haiwezekani.

217 Sasa, mimi ni mmishenari, nami nimekuwa kote ulimwenguni, katika aina yote ya maovu, na namna zote za wanaoamini mizimu, na na makundi makundi, na namna zote za ibada za shetani, na, ee, kila kitu kinachoweza kuwaziwa, ambapo kuna kila kitu, nami kila mara nimetambua kuwa wema daima hushinda uovu.

218 Sikiza, sijali usiku ni mweuzi vipi; huenda ukawa mweusi sana hata ungeugusa; ungeinua mikono yako juu hivi na hungeona kivuli cha namna yo yote. Nuru ndogo mno itafichua hilo giza. Hakika, hivyo ndivyo uzima ufanyavyo mbele ya giza. Hivyo ndivyo kweli ifanyavyo mbele ya uongo. Hivyo ndivyo imani ifanyavyo mbele ya mashaka, inayatawanya.

219 Usiku unawezaje kukaa hapa hali jua linang'aa—linaangazisha baraka? Usiku huenda wapi? Haupo tena. Usiku unakuwaje? Giza hilo liko wapi lililokuwa katika maskani haya yapata masaa kumi na mawili yaliyopita? Liko wapi giza lililokuwa limejaa ndani ya kuta hizi hapa? halipo tena. Limetoweka. Mbona? Nuru iliingia. Na nuru ilipoingia, giza lilipaswa kuondoka.Naam, bwana!

220 Chukua viumbe wanaotembea usiku, kombamwiko, na mende, na kunguni na kadhalika. Acha jua lichomoze au acha nuru iwamulike, tazama jinsi wanavyokimbilia gizani. Hivyo ndivyo Injili ilivyo. Inapoangaza, inakuwaje kwa wale wanaotaka kuwaita ninyi watakatifu wanaojigaragaza? Inakuwaje kwa watu wale wanaowadhihaki ninyi, Nuru inapoangaza, wanatimua mbio kuelekea gizani wamenyamaa wawezavyo, kwa sababu wao—wao ni wana wa usiku. Lakini wana wa mchana huenendea Nuruni.

221 Basi sisi ni wana wa Nuru kwa neema ya Mungu. Kwa hivyo Nuru inapoangaza, tunamshukuru Mungu na kutembea tukiwa macho, tukivitazama vitu ambavyo hamwezi kuviona kwa macho yetu ya kawaida. Naam, imani ni kuwa na hakika

ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana. Amina! Napenda hilo.

222 Sina wakati kwa ajili ya mahubiri yangu madogo ambayo nilikuwa nataka kuyahubiri, kwa sababu tutawaombea wagonjwa.

223 Wangapi wanampenda Bwana? Amina! Sasa, baada ya sisi kuwa na maswali haya, na kuna mengine makali na kila kitu, na yanaweza kujibiwa . . . Labda hata sikufanya kazi hiyo vyema, kwa sababu sikuwa na wakati kuyachunguza Maandiko. Na ningeyaandika kwenye karatasi kama ningalikuwa nao. Natumai kila mtu ametosheka. La. sivyo, naam, liandike kanitumie. Hebu nipate wakati kulisoma kirefu ukidhani halikujibiwa kabisa.

224 Asanteni kwa kuketi. Na sasa, tutafanya mstari wa maombi hivi punde. Lakini kabla hatujafanya hayo, hebu sasa tugeuze hali ile toka kwa majibu na mmoja akijibiwa hivi, na mwingine akiamini hivi na vile. Mwaona, katika kujibu maswali, wakati mwingine ni kali kidogo, kwa hivyo hebu tumwabudu Bwana tu na kuimba.

Nampenda, Nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Sasa, ninataka msalimiane kwa mikono na mtu mwingine karibu nawe tunapoimba tena.

Nampenda, Nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Sasa, hebu tuinue mikono yetu Kwake hivi, tufunge macho yetu.

Nampenda, Nampenda,
Kwani alinipenda kwanza,
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

225 Baba yetu uliye Mbinguni, tunakupenda Wewe Bwana. Nami naamini hili kundi ndogo linakupenda Wewe. Tunakuja huku katika hii nyumba ya Mungu Aishiye, jengo ndogo, si jengo, lakini Mungu aishiye humu jengoni. Kama vile ndani yangu, maskini mwili huu, hapana budi utaanguka hivi karibuni, lakini mtu anayeishi ndani yake hawezi kuanguka, kwa sababu ameshikiliwa na nguvu za Mungu.

226 Hili jengo zee hapa tunaloabudia asubuhi hii, haijalishi jinsi tunavyolitengeneza, siku moja litaanguka, lakini Mungu anayeishi humu jengoni ni wa milele. Tunakuja Mbele Zako sasa, Baba, kukupa shukrani na sifa.

227 Na kwa maswali haya yaliyo katika mioyo ya watu, twaona kuwa wao walikuwa wakishangaa kama wao wanapaswa kufanya *hili* au *lile*. Basi, Baba, natumai kuwa katika kila moyo mwepesi wa Mkristo ya kwamba jibu lilikuwa hivi kwamba lingewafanya wao wafahamu yaliyo kweli. Tujalie, Bwana. Na kama nilishindwa, basi nisamehe. Sikukusudia kushindwa, kwa sababu ni watoto Wako, nao wanauliza maswali hayo. Nami ni—ninataka kuwapea yote nijuayo, Baba, kama kwamba Wewe ulikuwa umesimama hapa kunihukumu kwa yale niliyosema.

228 Sasa, Bwana, tunakuja kuwashughulikia wagonjwa. Sasa, tunajua ya kuwa katika Biblia tunapata tu yale tunayoamini tutapata. Tunakumbuka wakati mmoja, Baba, Yesu alipokuwa hapa duniani. Yule mwanamke Msirofoinike alimjia na kusema, "Bwana, umrehemu binti yangu, kwa sababu amepagawa sana na pe—pepo."

Na tunasikia yale Yesu alisema, "Si vema Kwangu kukitwaa chakula cha watoto na kuwatupia mbwa."

229 Ee, Mungu, yaonekana kuwa ni ku—kukataa kabisa, isitoshe, kumwita mwanamke yule mbwa. Lakini badala ya kujivunia hayo, kwa upole na unyenyekevu yeye alisema, "Hiyo ni kweli, Bwana." Kwa sababu ilikuwa Kweli. Mwanamke yule alisema, "Ndiyo, Bwana, lakini hata mbwa hula makombo yaangukayo toka mezani pa bwana zao." Hilo ndilo lililotenda kazi. Yeye alikuwa tayari kuchukua makombo yaliyotoka mezani pa watoto. Basi Mungu, hiyo ndiyo nia yetu hivi sasa. Tuko tayari kwa cho chote ambacho Wewe unataka kufanya nasi, Baba. Sisi tuko mikononi Mwako.

230 Nina furaha sana kujua kwamba Mungu wa Agano la Kale, aliyetuonyesha maono na kutupea ishara na maajabu, yuangali hai leo. Na Mbinguni wanakotarajia kuenda, wakati mmoja kwa neema ya Mungu tutaenda pia, kwa sababu Mungu yule yule anajidhihirisha Mwenyewe kuwa Mungu yule yule kati yetu.

231 Kunao wale kati yetu, Baba, asubuhi hii ambao ni wagonjwa na wahitaji. Watapitia katika mstari wa wanaohitaji maombi. Hebu wasije wakasema, "Vema, siamini kuwa wewe unanweza kunifaa kamwe. Ni—ni . . . " Bwana, hebu hiyo isiwe ndiyo nia, bali hebu waje wakikumbuka kuwa Mungu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Uliahidi hayo; ulisema hivyo.

232 Hebu wao waje kwa utulivu mtakatifu, wakiamini kuwa mara tu ombi linapotolewa na mikono imewekwa juu yao, basi Roho Mtakatifu atawashukia kama huyu dada mpendwa aliyeandika swali lile, kasema, "Roho Mtakatifu nusura aangamize nafsi yake kwa ubatizo mkuu ajabu wa uwepo Wake."

233 Hebu hayo yawe—hebu hayo yawe matokeo kwa kila mmoja ajaye asubuhi ya leo, Bwana. Tujalie. Hebu wao na waponywe.

Hebu wao waje wakijua, wakijua ya kwamba bila shaka kabisa Wewe uliahidi hayo na hauwezi kusema uongo, na mara tu nuru inapogusa, giza na tashwishi hutoroka. Tujalie, Baba. Tunawaweka Kwako sasa tunapowaombea katika Jina la Yesu. Amina!

234 Sasa wale wanaotaka kuombewa, upande huu kwanza, simameni jengoni hapa, huku Teddy anapotupigia, *Ni Tabibu Wa Karibu*. Njooni humu, rudini nyuma, wengine wao *hapa*.

Ni tabibu wa karibu . . .

235 Ndugu Neville. Endelea tu kuwapanga, huku wanakuja. Tutasimama hapa. Hebu kanisa lote liendelee kuomba. Nami na Ndugu Neville tutakuwa hapa pamoja; yeye atakuwa akiwapaka mafuta, nami nitawawekea wagojwa mikono, papa hapa mbele. Sasa, kila mmoja aendelee kuomba sasa.

236 Tunafanya nini? Tunakuja kuwapaka wagojwa mafuta na kuwaombea. Hebu sasa niwanukuulie Maandiko. "Kama kuna mmoja kati yenu, aliye mgojwa, na awaite . . . "

[Mahali patupu katika ukanda . . .

237 Ilitendeka kikamilifu tu, jinsi hasa ilivyokuwa. Nilikuwa nayo, huku nikitetemeka, nikiwazia. Ona? Labda . . . Nikasema, "Labda ilinipasa kuwaambia hiyo ingekuwa hivyo." Lakini, nilisema, "Vema, hebu iache tu."

238 Nayo hutendeka kila siku, ona Jambo fulani litatendeka, naliacha tu litendeke. Mungu anajua hiyo ni kweli. Ona? Jambo tu litakalotendeka, linajionyesha, linalisema. Jambo fulani litanijia, na kusema, "Sema tu neno hili hivi, na jambo hili litatendoka humu." Kisha nitasema, "Vema, hebu iwe hivyo." Kisha nitachunguza, ndilo hili hapa. Ona? Naam.

239 Vema, kama Yeye anaweza kufanya vitu, vitu vya kuonekana, kitu kisicho na uhai, kiende kulingana na Neno Lake, kwa sababu tumesema, ni zaidi sana Yeye awezavyo kuwafanyia ninyi mnayeshirikiana nami. Ninyi mko pamoja nami, ninyi ni ndugu—ninyi ni ndugu na dada zangu walio wagojwa. Na kama tukisema maneno haya, "Hebu na nguvu za Mungu zimponye mtu huyu," naam, haina budi kutendeka. Sasa, kitu hicho hakiwezi kusema, "La, naona shaka." Itaenda na kulifanya. Bali unaweza kusema, "Vema, nashangaa," na haitatendeka, ona. Bali ukiendelea tu na kushikilia wazo lako sasa, "Nitaponywa," huna budi kupona. Unaamini hilo?

[Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

240 Basi, hebu sote tuombe. Baba yetu wa Mbinguni, namwekelea mikono maskimi bibi huyu, maskini mama huyu anayesimama hapa . . .

241 [Mahali patupu, huku Ndugu Branham na Ndugu Neville wakiendelea kuwaombea wagojwa—Mh.]

242 Na kwa hivyo naomba ya kwanba Wewe utawaponya watu ambao watawekelewa leso hizi. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

243 Tunawashukuru sana kwa kukaa kwenu, na uaminifu wenu kukaa wakati huu wote, na kungoja kanisani hivi, huku sisi... Bali sijui mahali pazuri zaidi pa kuweko, nanyi je, kuliko kanisani?

[Kusanyiko linavema, "Amina."—Mh.] Sijui mahali pazuri zaidi pa kuweko. Na faraja tuliyo nayo ya kwamba Mungu... ya uwepo Wake sasa.

244 Nasi, kwa muda kidogo tu, na tuwazie jinsi Yeye alivyo mkuu, na yale aliyotutendea. Tungefanyaje bila Yeye? Jinsi tumemwona Yeye, hamna jambo moja alilopata kutuambia kupitia kwa...Alinipa maono. Nami nawaulizeni, asubuhi ya leo, je, mmekwisha kuona moja isipokuwa lile alilotimiza? Jinsi hasa Yeye alisema angefanya, wakati uo huo. Basi, Yeye ni Mungu. Basi, Yeye ni Baba yetu. Yeye anatupenda. Na po pote Mbinguni Yake ilipo, mnajua hatuna budi kwenda kule siku moja. Tunajua Yeye yuko sasa. Tunatambua hilo.

245 Sisi, tunatazama mambo ambayo hatuoni. Sasa wengi wenu waliombewa, na, mnaona, tunakataa dalili yo yote dhidi yake. Ona? Cho chote ambacho Mungu ameahidi, ona, Mkristo hatazami...Huoni kwa macho yako haidhuru. Unajua hivyo. Huoni kwa macho yako. Unaona kwa moyo wako. Ona? Kuona maana yake ni "kufahamu." Unafahamu kwa moyo wako, kwa hivyo sisi huangalia vitu ambavyo macho yetu hayaoni. Ona? Kukiri kwa Mkristo, silaha zote za Ukristo, zinategemea hilo. Sisi, sisi hutazama mambo ambayo hatuyaoni, kwa kuwa Ibrahimu aliviita vitu hivyo ambavyo havikuwepo kana kwamba vilikuwepo, kwa sababu alimwamini Mungu. Ona?

246 Basi tufanyeje sasa? Sasa wakati unapoombewa hivyo, basi Mungu aliahidi kukuponya. Basi sasa hivi huenda usisikie tofauti yo yote, bali Yeye...Hilo, sivyo ilivyo kamwe. Ona? Tunaamini, haidhuru.

247 Laiti mngalijua, nilikuja mimbarani yapata masaa mawili yaliyopita nami sikufikiria ningefikia nusu ya mkutano, karibu nusu. Nalikuwa mchofu na msumbufu, nami nikajisikia kama ningeugua mafua, bali sasa najisikia ajabu kwa kuwa nilisema, "Ninapasiwa kwa Mungu. Namwamini Mungu." Nami ilinipasa kupigana naye. Mke wangu pale angewaambia vivyo hivyo, kwa kujaribu kushika njia nije humu asubuhi ya leo, nami nilikuwa nimepwewa sauti kooni mwangu na kila kitu. Nikasema, "Nitawezaje kufanya hivyo?" Bali, hakika, najisikia vizuri sana sasa. Nami na—naamini ningechukua somo langu na kuhubiri, na—na nijisikie tu vizuri.

248 Lakini, kwa sababu, unaona, huna budi kutazama vitu hivyo ambavyo huvioni kwa macho yako. Unaviona kwa moyo wako.

Unaamini, nawe unatoa ushuhuda juu ya vitu hivyo ambavyo huvioni, bali vile ambavyo unaamini. Kwa sababu ni imani. "Na imani ni kuwa na hakika ya manbo yatarajiwayo, ni bayana ya manbo yasiyoonekana."

249 Nimemtazama, asubuhi ya leo, kijana Mkristo ambaye amekuwa akiketi hapa mbele yangu. Nami najua maamuzi ambayo mtu huyo alifikia. Bila shaka nathamini hayo. Singesema ilikuwa nani, bali ni—ninathamini—uamuzi Mkristo huyu aliofikia, haijalishi kama ingekuwa mwenziwe, rafikiye, baba au mama yake, ama ye yote yule, wao wana hamu ya kudumu waaminifu kwa Kristo. Ona?

250 Hiyo ndiyo njia ya kumpata mtu unayempenda. Kuwa mwaminifu ndiyo njia tu ya kumpata mtu umpendaye. Shikilia imani yako. Hakikisha ya kwamba wewe u mwenye haki mbele ya Mungu, kisha udumu huko daima. Shikilia hilo tu.

251 Sasa, sisi sote tutafanya makosa. Kumbukeni tu. Na mnapoangaliana, usiyatazame makosa ya mtu mwingine. Ona, usifanye hivyo, kwa maana, kumbuka, unafanya makosa, pia. Bali mtazame Kristo ambaye anamwongoza mtu huyu. Na iwapo wanataka msaada, Basi wewe waombee. Hivyo, hivyo ndivyo tunavyoendelea, ona, omba. Na, kumbuka, unapomwombea mtu mwingine katika shida kama hiyo, Mungu atakusikia na kukuponya unapomwombea mtu mwingine. Hiyo ni kweli. Huo ndio msingi wa Ukristo, kusaidiana, kutendeana, kuhurumiana, kuelewana. Sasa, ukiona kosa la jirani yako, unaona mahali wamekosea, usikosee pamoja nao, bali waombee tu. Endelea kuomba, naye Mungu atafahamu hilo. Atatengeneza mambo yote.

252 Sasa, minatumainia, Bwana akipenda, nafikiri Billy ana mpango fulani, yeye humtumia kila mtu kadi. Na kama mama atapata nafuu juma hili; na kila kitu, Jumapili ijayo. ni—nitahubiri U—Ujumbe wa Injili. Iwapo hiyo ni sawa kwa m—mchungaji wetu hapa. Basi tunatarajia ya kwamba mtarudi mkiweza. Mkiweza kuja, tutafurahia kuwa pamoja nanyi.

253 Je, mnampenda kwa moyo wenu wote? [Kusanyiko linajibu, "Amina."—Mh.] Si Yeye ni wa ajabu? Tungelifanyaje pasipo Yeye? Naam, tungefanyaje? Waweza kuniambia cho chote ambacho kingekuwa kikuu zaidi? Kama waweza kunionyesha cho chote kilicho kikuu kuliko hicho, basi ni—ni—nitauza niliyo nayo, kisha niwe na shauku ya hicho ulichonionyesha ambacho ni kikuu kuliko Hili. Naam, bwana. Hili ndillo jambo kuu sana nijualo, kujua yakini ya kwamba tumeokolewa, kujua ya kwamba Mungu yule yule aliyeumba mbingu na nchi angejidhili nafsi Yake na kushuka na kuishi kati yetu, na kutufanyia.

254 Sasa hivi ndivyo tujuavyo kama tuko sahihi au la, ona, kwa maana jambo lile lile alilofanya, hapo mwanzo, pamoja na wale Wakristo kule nyuma, kanisa lile lile, kutenda kazi kule

kule, jinsi Roho Mtakatifu alivyotenda kazi, na jinsi shetani alivyopigana nao, na jinsi wao walivyosimama, hilo ndilo jambo lile lile linalotendeka papa hapa, kwa ishara zile zile, maajabu yale yale, Mungu yule yule, thibitisho Lake lisilokosea.

255 Niambieni, katika ulimwengu wa sayansi, niambieni kwa njia ya sayansi, jinsi mtu ye yote angetabiri jambo ambalo lingetendeka katika miaka ama nyakati zijazo, kabla halijatukia. Nionyeshe huo uweza, ambapo huo ungekuwa, ambao ungejua hilo kabla halijatendeka. Niambie akili ya mwanadanu ambayo ingerudi nyuma kupitia kwa cho chote utakacho, na nionyeshe njia yo yote ambayo ungeona jambo fulani na kutabiri jambo fulani, ambalo lilitendeka jinsi tu—jinsi tu lifanyavyo. Ona? Hamna.

256 Kwa hivyo, Yeye ni Mungu. Ona, Yeye ni Mungu. Na kwa kuwa Yeye ni Mungu, kwa neema Yake anakuja na kuishi ndani yetu, na jinsi tu alivyofanya na hao watu kule nyuma waliotabiri mambo haya, na kila moja ya haya yakatendeka jinsi tu yalivyotabiriwa Sasa, Mungu yuyo huyo yuko pamoja nasi, akitabiri na kuonyesha mambo yale yale aliyotenda kule nyuma. Naam, inatupasa tuwe na furaha sana, tungekuwa tukirukaruka kama kutoka wingu hata wingu, hivyo, karibu tutembee tu hewani, kwa sababu tunajua.

257 Tunajua ya kwamba tumepita mautini kuingia Uzimani. Tunajua ya kwamba tuna wokovu. Tunajua ya kwamba sisi ni Wakristo. Na tunajua ya kwamba tunaenda Mbinguni, kwa sababu Mungu alitufanyia ahadi, na ndiye huyu hapa anatembea kati yetu, na kwa njia ambayo tunamwona.

258 Tunamwona. Ninamwonaje? Ninapowaona ninyi. Ninyi mnamwona Yeye ndani yangu; mimi ninamwona Yeye ndani yenu. Ona, ninaona yale Yeye anawatendea. Sasa hapo namwona Yeye akinifunulia Neno. Unasema, "Unawezaje kumwona ndani yangu?" Vema, tazama, Yeye yuko hapa akinifunulia mimi Neno. Naiona kule, Yeye akikupa wewe, nawe ukiliweka. Unaona? Kisha unatazama nyuma, na kusema, "Aliwezaje, hilo lilipataje kuja?" Kisha unarudi, unaoma ya kwamba hiyo ni kweli, ona. Kwa hivyo unamwona Yeye ndani yangu, mimi ninamwona ndani yako.

259 Nasi tunaweza kumwona katika mapambazuko. Tunaweza kumwona katika magharibi. Tunaweza kumwona katika maua. Tunaweza kumwona katika—tunaweza kumwona mahali po pote, kwa kuwa tumepita kutoka vitu vya hali ya chini ya hali hizi za kilimwengu, tukaingia katika mambo ya hali ya juu ya utukufu wa Mungu, kusudi tupate kuona Uzuri Wake.

260 Siku chache zilizopita, nilipokuwa katika safari hii, kwenye—kwenye Barabara Kuu ya Alaska, nilipoenda kuwinda, nilirudi kule nikishangaa, "Kwa nini? Kwa nini?" Nikatazama

jinsi—jinsi Mungu alivyo halisi. Sasa kuna wagojwa kila mahali, hata hivyo Mungu anajua.

261 Sasa, kesho ninaturajiwa kuondoka kwenda Colorado, kwa ajili. . .kwenda kuwinda kila mwisho wa mwaka ambapo. . . nimetoka mikutanoni, kuenda. Siwezi kwenda, kwa sababu ya mama, hali ya mama.

262 Sasa tazama wema wa Roho Mtakatifu. Yeye alijua hayo muda mrefu uliopita. Kwa hivyo, badala ya kuniacha niende, akageuka akanipa ono na kunituma humu, kisha akanipa safari ya uwindaji ambayo singeipata Colorado, ona, maana hao wanyama hawako Colorado hivyo. Nikageuka, kisha akanipa hiyo kwa ono, na kunipa hilo, akijua angepaswa kunifanya nisifanye hii safari ya Colorado. Nena habari za wema na rehema! Basi kwa nini? Halafu, kwa muda mrefu, Yeye alijua mama yangu angepata maumivu. Alijua ya kwamba mama yangu angekuwa hospitalini. Kama akiruhusu, anafanya hivyo kwa kusudi zuri ambalo sijui cho chote juu yake. Bali najua yote "yanafanya kazi kwa wale wampendao Bwana katika kuwapatia mema."

263 Laiti tungalikoma mara kwa mara, enyi kanisa, tupate kumwona Mungu wetu! Hebu tulia tu uondokee masumbuko yako, ukasimame kimya kwa dakika chache katika Uwepo wa Roho Wake, nawe unaweza kumwona tu akitenda kazi kila mahali. Mnaona jinsi alivyo mzuri?

264 Sasa ndiye huyo mama amelala pale, huku nikishangaa juu yake. Mbona Yeye hakumwacha aage dunia *alipozirai*? Mbona hakufa papo hapo? Lakini, mnona, kwa kuwa Yeye alijua hayo hapo mbeleni, na akijua ya kwamba nilikuwa nimeahidi ku-. . . Nilikuwa ninaenda kule Colorado, na alijua ya kwamba mimi hupenda kwenda mwituni hivyo, Yeye aligeuka tu akanipa kitu bora zaidi, akanituna humu, kisha akaniambia nitakachopata, na kila kitu juu yake, kabla hata sijaondoka; akaniambia jinsi watu wangevalia nguo, na yale tungefanya, kila kitu. Kisha nikaja, nikawaembieni nyote. Kisha anaenda kule na kuona hayo yakitendeka, akarudi, jinsi alivyosema hasa. Hivyo hasa, mwaona, akijua ya kuwa huyo mama angekuwa huko, akijua ya kwamba yeye—yeye angezirai wakati huu, nami songeweza kufanya safari hii nyingine. Ona? Hatungefa-. . .Sikufahamu hilo, mimi binafsi, wakati huo. Bali ukijitolea mwenyewe Kwake na kumtazama, Yeye huongoza kila kitu sawa kabisa. Ona, Yeye huyafanya yote kutendeka sawasawa, hatua kwa hatua.

265 Hivi majuzi, nilikuwa nimesimama karibu na kijana muhudumu aliyeota doto kadhaa, kisha akaniletea hizo doto. Wakati tafsiri ilipotolowa, tulisimama pale, mimi na Billy na huyu muhudumu, tulisimama pale pamoja. Ndiyo hiyo. Naam, ilikuwa tu kamilifu iwezavyo kuwa. Na jinsi mtu huyo alisimama hapo kwa—kwa—kicho, na jinsi alivyoona kwamba

Roho Mtakatifu angefunua mambo hayo, na kumrudisha nyuma na kumwonyesha kule barabarani hasa na ambako inapaswa kutendeka. Lo, nawaambieni, Yeye ni Mungu. Yeye, Yeye yu hai . . . Yeye ni Mungu.

266 Watu wengi sana wamejitolea. Mmewaacha marafiki wenu wavulana kwa wasichana, mmeziacha nyumba zenu, na kadhalika, wengi wenu imewalazimu kuwaacha wenzenu na marafiki zenu, na kadhalika, na marafiki wa kale ambao mmewajua kwa muda mrefu sana, kutembea katika njia ya Bwana. Ninawapongeza kwa ajili yake. Nafikiri ni vizuri sana kufanya hivyo. Sasa kwa sababu mumeona Huru ya Injiri, na ni Kweli, nanyi mna—mtatembea katika hiyo Nuru. Na cho chote mfanyacho, enyi watoto, cho chote mfanyacho, po pote mwendapo, jiepusheni na uovu wa kila namna, mumfuate Kristo. Mradi tu mko hai, shikeni tu njia. Msiondoke kwake, bila shaka itawafaidi. Ni Uzima wa Milele.

267 Nami nimemwona mama wakati—kila anapo-. . . anaweza kujirudia kwa dakika chache. Kasema, “Mama, mama, unanisikia?” Wakati mwingine amelala pale tu, hatanisikia. Kisha baada ya muda kidogo atasema, “uh,” anatikisa kichwa chake *hivyo*. Nitasema, “Je, una-. . . ” Nikasema, hivi majuzi usiku, nilisema, “Mama, unanijua?” Hakunijua. Nikasema, “Je, unajua ni nani huyu anayesimama hapa?” La, hakujua hilo. Nikasema, “Mama, unamjua Yesu?” Naye . . . Lo, jamani! Huenda akasahau mtoto wake, bali hawezi kumsahau Yesu. Ndivyo ilivyo. Lo, ndugu!

268 Haujui maana ya hayo hata yanapowapata jamaa yako binafsi, kufikia hayo, mwaona. Kumjua Yeye ni Uzima. Kumjua Yeye ndiko ridhaa ya kujua, maisha haya yatakapokwisha, tuna makao kule ng’ambo za mbingu. Kwamba hiyo ni nini, sijui. Sijui jinsi ya kuwaambieni itakuwa, kwa maana sijui, mimi binafsi. Bali najua ya kwamba siku moja, kwa neema ya Mungu, tutasafiri Huko.

269 Niombeeni juma hili. Nayahitaji. Na sasa niombeeni; nitawaombea. Bwana akipenda, akinijalia, nitakutana nanyi Jumapili ijayo. Basi kumbukeni ibada ya jiomi hii. Huenda ikawa, iwapo haitanilazimu kuketi usiku huu, ama cho chote kile, na niwe kule na mamangu, labda nitakuwa pamoja nanyi usiku huu.

270 Na sasa, Ndugu Neville, mchungaji wetu wa thamani, njoo humu. Sijui vipi bila shaka . . . Hamna mtu hapa ila watu wa nyumbani, mwajua. Sote tunajiita watu wa kinyumbani. Nathamini msimano wa Ndugu Neville kwa ajili ya Ukweli huu wa Injili. Nathamini uaminifu wake na unyofu wake mbele za watu. Na hivi majuzi, alipokuwa akinena; sikuwa nimeona hilo kamwe, bali alipokuwa chini ya upako, akitoa unabii, yeye aliniita nabii, chini ya upako. Huyo hakuwa yeye akiniita wakati

huo, huyo alikuwa Roho Mtakatifu. Kwa hivyo hilo lilinipa ujasiri na imani ya kusonga mbele, kwenye vilindi vyenye kina kirefu na vimo vya juu zaidi, pamoja na Mungu. Nakuthamini, Ndugu Neville. Mungu akubariki. Na hata nitakapowaona tena, Mungu awe nanyi.

*Mwenendo, Utaratibu Mafundisho ya Kanisa*, Kitabu Cha Pili
(Conduct, Order And Doctrine Of The Church, Volume Two)

Jumbe hiza za Ndugu William Marrion Branham, ziliohubiriwa hapo awali katika Kiingereza katika Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, hapo awali zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org